# Nipashe

Jumanne Mei 2, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581298


www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



MID WEEK JACKPOT!
TZS. 567,947,180
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

## Utouh amsifu mkulima kushtaki aliowataja CAG

UKURASA 5




UKURASA 11



# NYONGEZA KIMYAKIMYA

• **Samia** atangaza mshahara mpya kila mwaka, aonya wafanyabiashara... *Uk. 2*



Wafanyakazi kutoka Wizara, Taasisi mbalimbali za Serikali na Binafsi, wakipita mbele ya Jukwaa Kuu kutoa ujumbe kuhusiana na masuala mbalimbali ya Wafanyakazi wakati wa Maadhimisho ya Sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi, ambapo Kitaifa yamefanyika Mkoani Morogoro jana. **PICHA: IKULU**

## ACT yatangaza utayari wake timu maalum hali siasa Z'bar

UK. 4

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

### NDOTO YA SAMIA KUIFUFUA

SERIKALI imeiwezesha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) Sh. bilioni 4.65 kununua vitendea kazi na ng'ombe wazazi ili kuboresha..

UKURASA WA 7

### MSTAAFU: BILA NSSF NINGEADHIRIKA

MWANACHAMA mstaafu wa NSSF, Anselmi Fungosita, ameushukuru Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa kuendelea kumlipa pensheni yake ya uzee kila mwezi kwa..

## Mvua ilivyoua bibi, wajukuu,mti wamwokoa mama yao

UK. 5

**MICHEZO** NABI AIGEUKIA MARUMO, UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Wafanyakazi wa sekta ya Uchukuzi wakishiriki katika maadhimisho ya sherehe za Mei Mosi, jana jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mishahara sasa kuongezwa kimya kimya

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ametangaza neema kwa wafanyakazi nchini ya nyongeza ya mshahara kila mwaka na kulipa malimbikizo katika kipindi cha bajeti ya mwaka wa fedha ujao.

Rais Samia alitangaza neema hiyo kwa wafanyakazi katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Mororogoro.

Rais Samia alisema ongezeko hilo la mshahara na marupurupu litapandishwa bila kutangazwa hadharani ili kuepuka wafanyabiashara wanaotumia mwanya huo kupandisha bidhaa.

Alisema tayari serikali ilishaongeza nyongeza ya asilimia 23 kwa wafanyakazi wenye mishahara ya chini na wameshaanza kunufaika na nyongeza hizo katika bajeti ya sasa.

"Tulishaongeza asilimia 23 ya mshahara kwa wafanyakazi wa chini na wameanza kunufaika na ongezeko hilo na kupandisha marupurupu kwa wafanyakazi wa ngazi ya juu, hivyo natumia nafasi kusema tutapandisha tena mishahara, lakini kimya kimya ili kudhibiti wafanyabiashara kupandisha bei ya bidhaaa," alisema Rais Samia.

Kadhalika, alisema serikali inatambua kuwapo madai ya wafanyakazi katika sekta zote na tayari imeshaanza kuhakiki na kulipa madai yao baada ya kujiridhisha na uhakiki wake.

Hata hivyo, aliagiza madai yote yaliyobaki ya wafanyakazi kuanzia sasa yalipwe ndani ya siku 90 baada ya kuhakikiwa ili kuongeza tija katika sehemu ya kazi.

Alisema serikali inathamini wafanyakazi na inakusudia kupandisha madaraja na vyeo vya mseleleko kila mwaka ili wafanyakazi waendelee kunufaika.

Kuhusu kodi, Rais Samia alimuagiza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kukaa pamoja na viongozi wa vyama vya wafanyakazi ili kuangalia namna ya kupunguza kodi zisizo na ulazima kuwaondolea kero wafanyakazi.

Alisema kwa hivi sasa serikali inafanya kila jitihada ya kuzungumza na kuvutia wawekezaji kutoka nje ya nchi wawekeze nchini ili kusaidia Watanzania kupata ajira.

Awali, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Henry Mkunda, alisema wataendelea kuunga mkono jitihada za serikali kuongeza ajira za Watanzania.

Mkunda aliomba serikali kuboresha kitengo cha Idara ya Kazi kwa kuwa hivi sasa kinafanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kukosekana kwa vitendea kazi na rasilimali watu. Akizungumzia kuhusu bima ya afya kwa wafanyakazi, alisema wapo baadhi ya waajiri licha ya kuwakata wafanyakazi hawawasilishi kwa wakati katika vituo vya kutolea huduma na kusababisha changamoto kwa wafanyakazi kushindwa kupatiwa huduma za afya.

**MWANZA**

Mkoani Mwanza maadhimisho hayo yamefanyika kimkoa wilayani Sengerema ambako wafanyakazi wametakiwa kuwa waadilifu na waaminifu katika sehemu zao za kazi ili kuleta ufanisi kazini na kuboresha hali ya utendaji kazi na huduma kwa wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alitoa rai hiyo ya kuwataka wafanya kazi wote kutimiza majukumu lengo likiwa ni kuinua huduma katika sekta binafsi na serikali kwa ujumla

Kadhalika alizitaka sekta binafsi kuendelea kuwaboreshea maslahi wafanyakazi wake kutokana na malalamiko ya kudorora kwa utenda kazi wa sekta hizo kwa sababu ya maslahi yao kuwa chini.

Katibu TUCTA Mkoa wa Mwanza, Zebedayo Athuman, alisema pamoja na serikali kuongeza mishahara bado haikidhi kuendesha gharama za maisha kwa sasa kwa kuwa kila kitu kipo juu na kuiomba serikali kuendelea kushughulikia suala hilo hususani katika kipindi hiki.

**ARUSHA**

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella ametoa siku saba, kwa Halmashauri za Karatu, Longido na Halmashauri ya Arusha, zinazolalamikiwa kutolipa wafanyakazi wake kwa mapato ya ndani, walipe madeni yote ndani ya siku hizo.

Aidha, ameiagiza Halmashauri ya Ngorongoro kuwalipa wafanyakazi bora wa mwaka jana zawadi zao hadi ifikapo Ijumaa, wiki hii.

Agizo hilo alilitoa jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, ambayo kimkoa yaliadhimishwa jijini Arusha na kuhudhuriwa na umati wa wafanyakazi, huku yakipambwa kwa ndege ya Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori (TAWIRI) iliyokua ikizunguka uwanja wa mpira Shekhe Amri Abeid.

Alisema ni vizuri kila kiongozi akawajibika katika eneo lake kwa kusimamia vizuri wafanyakazi wake.

Kuhusu wafanyakazi bora kutajwa kwenye maadhimisho halafu waajiri wanawarusha au kuwapiga danadana wafanyakazi hao, alisema hapendi kulisikia likijirudia na halikubaliki.

"Kwa kuwa Ngorongoro imelalamikiwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), nawaagiza hadi kufika Ijumaa wiki hii, muwe mmelipa stahiki zao wafanyakazi wenu bora wa mwaka jana na sio mkiwalipa hao iwe sababu ya kutolipa wengine wa mwaka huu, hapana, mliwajua na kila mwaka mnajua kuna siku hii na hii kwa wote mnaowataja wafanyakazi bora halafu mnakaa kimya, sitataka kusikia. Ni bora msiwataje," alisema.

Aidha kwa sekta binafsi, alizitaka lazima zifuate maazigo ya serikali ya ulipaji wa kima cha chini cha mishahara, kwa kutofanya hivyo ni kukiuka maagizo ya serikali.

Pia, kampuni zilizofungwa yakiwamo mashamba ya maua na kudaiwa na wafanyakazi wao, alishauri menejimenti zao zifuatwe kufahamu zaidi shida zianazowakwamisha kutekeleza hilo.

Alionya waajiri hasa wa sekta binafsi wanaozuia kuanzishwa kwa matawi ya vyama vya wafanyakazi wahakikishe yanakuwapo, kwa kuwa sio takwa la mtu, bali ni sheria ya nchi na kwa kuzuia ni ukiukwaji.

Mwenhekiti wa TUCTA Mkoa wa Arusha, Lotha Lazier, alilalamikia Halmashauri ya Karatu, Jiji Arusha na Karatu, kuwachelewesha stahiki wafanyakazi wao wanaolipwa kwa mapato ya ndani na kusababisha adha kubwa kwao, huku Halmashauri ya Ngorongoro ikiwapiga danadana wafanyakazi bora wa mwaka jana kuwalipa stahiki zao.

Mratibu wa TUCTA Mkoa wa Arusha, Daud Kamwela, aliomba serikali kuhakikisha wastaafu wa sekta binafsi wanapata huduma ya Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) kama ilivyo kwa wastaafu wa sekta ya umma kwasababu wote wanachangia.

"Kitendo cha kuwanyang'anya wastaafu wa sekta binafsi vitambulisho vya bima ya afya, huku wakiachiwa wale wa sekta ya umma, ni ubaguzi tunaomba hili lifanyiwe kazi, kwani wote wamechangia wakiwa kazini," alisema.

**RUKWA**

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Qeen Sendiga, amewataka wakurugenzi wa halmashauri zilizoko mkoani humo kuwaepushia maradhi ya kudumu na vifo vya ghafla baadhi ya wastaafu kutokana na kutowalipa kwa wakati stahiki zao.

Sendiga alisema kitendo cha waajiri kutowalipa kwa wakati wastaafu ambao walikuwa sehemu ya watumishi wao kumesababisha wengi wao kubaki wakidhalilika mitaani na wakati mwingine kufariki kabla ya muda wao kutokana na kupata maradhi mbalimbali.

Alisisitiza wafanyakazi wengine wanaodai madai yao, walipwe kwa wakati ili kuondoa manung'uniko sehemu za kazi ambayo yanayosababisha kukosekana kwa ufanisi kazini.


Awali, Katibu wa TUCTA Mkoa wa Rukwa, Amini Msando, alisema watumishi wa umma mkoani humo wana madai ya stahiki zao za muda mrefu ikiwamo fedha za likizo na malimbikizo ya mishahara.

***Imeandikishwa na Ashton Balaigwa, MOROGORO, Elizabeth Seleman, SENGEREMA, Cynthia Mwilolezi, ARUSHA na Gurian Adolf SUMBAWANGA.**

TANGAZO

IPP
Cares For You

# Hakika Ameacha Alama



# ACT yataka timu maalum ya kufuatilia hali ya kisiasa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ACT Wazalendo kimeahidi ushirikiano katika kuundwa kwa timu maalum kutoka vyama vikuu vya siasa Zanzibar ili kuyafanyia kazi masuala yanayohusu demokrasia na hali ya kisiasa Zanzibar.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Salim Bimani, Katibu wa Habari, Uenezi, Mawasiliano na Umma wa chama hicho Zanzibar, alisema chama chao kinawahakikishia watanzania wote kitatoa ushirikiano kufanikisha kuundwa kwa timu hiyo na katika kuyafanyia kazi masuala yaliyokusudiwa ili kujenga misingi madhubuti ya demokrasia, umoja wa kweli na amani ya kudumu inayotokana na utendaji wa haki.

Alisema kuwa Kamati ya Uongozi ya chama hicho imemwelekeza Kiongozi wa Chama, Zitto Kabwe, kufuatilia uamuzi wa Kamati Kuu uliotaka viongozi wa kitaifa wa chama kukutana na Rais Hussein Ali Mwinyi ili kujadili kwa kina suala hilo na mengine yanayohusu maslahi ya Zanzibar.

Bimani alifafanua kuwa wakati anazungumza na vyombo vya habari Jumamosi iliyopita, Rais Dk.Mwinyi, alisema ameunda timu maalum kutoka vyama vikuu vya siasa Zanzibar; CCM na ACT Wazalendo ili kuyafanyia kazi masuala yanayohusu demokrasia na hali ya kisiasa Zanzibar.

Alibainisha kuwa baada ya kauli hiyo, waandishi kadhaa waliwasiliana na viongozi mbalimbali wa ACT Wazalendo kwa madhumuni ya kutaka uthibitisho wa suala hilo.

"Jana (juzi) Kamati ya Uongozi ya chama chetu ilikutana na tumejiridhisha kwamba, pamoja na kutambua nia na kuanza mchakato tokea mwezi Februari 2023 utakaopelekea kuundwa kwa kamati ya namna hio, kwa upande wetu hakuna taarifa kuwa timu hiyo imeshaundwa.

"Tulitarajia kwamba Kamati hiyo iwe imeshaundwa tokea mwezi Februari mwaka huu na kuanza kazi na kwa sasa iwe imeshakamilisha kazi zake. Hivyo, tunaikaribisha kauli hii ya Mheshimiwa Dk. Hussein Mwinyi na kuamini kwamba itaharakisha hatua ya kuundwa timu hiyo na kuanza kufanya kazi bila ya kuchelewa zaidi," alisema.

Bimani alisema tayari miaka miwili na nusu imeshapita tangu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na muda uliobaki kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2025 si mrefu huku mazingira yaliyosababisha shida mwaka 2020 yakiwa hayajabadilika kwa vile hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kuyabadilisha.

Alisema ACT Wazalendo inaamini hatua za kufanya marekebisho makubwa ya mifumo na sheria za uchaguzi ikiwamo Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), marekebisho ya mahakama na mfumo wa hakijinai Zanzibar.

Pia alisema wanaamini katika marekebisho ya idara maalum na vyombo vingine vinavyohusika na ulinzi na usalama Zanzibar, uimarishaji wa muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, na masuala ya kulipwa fidia waathirika wa matukio mbalimbali ya uvunjwaji wa haki za binadamu yaliyotokea mwaka 2020.

Alisema marekebisho hayo yanapaswa kufanyiwa kazi kwa haraka, kwa kina na kwa uadilifu ili Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ziepuke fedheha na maafa kama yale yaliyoshuhudiwa katika vipindi vilivyopita.



Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani kanda ya Afrika Mashariki, Jealous Chirove akitoa hotuba siku ya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, ambapo ameiomba serikali kurejea mikataba na kurekebisha sheria za kazi na kanuni ili kuongeza tija mahala pa kazi. Maadhimisho hayo yalifanyika kitaifa mjini Morogoro jana.**PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# CRDB yapata faida ya bilioni 133/- robo ya kwanza 2023

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB, moja kati ya taasisi kubwa zaidi za kifedha nchini, imetangaza kutengeneza faida ya Sh. bilioni 133 kabla ya kodi katika robo ya kwanza mwaka 2023.

Faida hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 3.1 kulinganishwa na iliyoipata kipindi kama hicho mwaka jana. Ufanisi huo, pamoja na mambo mengine, ukitajwa umechangiwa na mapato halisi ya riba yaliyofika Sh. bilioni 192 yakiongezeka kwa asilimia 9.7 kutoka mwaka jana.

Akizungumza kuhusu ufanisi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CDRB, Abdulmajid Nsekela alisema jana kuwa unadhihirisha uimara wa benki sokoni ambayo inatekeleza mpango mkakati wake wa muda wa kati kuanzia mwaka 2022 mpaka 2027, ambao inalenga kuuendeleza kwa kuwekeza zaidi kwenye fursa zinazojitokeza katika ukanda wa mashariki mwa Afrika hasa kwenye sekta za kipaumbele.

Aliema kuwa mapato yasiyo ya riba yalifika Sh. bilioni 106 katika robo ya kwanza, sawa na ongezeko la asilimia tatu kutoka Sh. bilioni 103 zilizopatikana mwaka 2022. Ongezeko limetokana na kuimarika kwa matumizi ya huduma mbadala hasa majukwaa ya kidijiti zikiwamo huduma za SimBanking, CRDB Wakala na huduma za benki kwa njia ya intaneti.

Vilevile, Nsekela alisema uwekezaji unaoendelea kufanywa na benki kwenye teknolojia, huduma za kidijiti pamoja na uboreshaji wa mfumo wa operesheni za benki utaimarisha huduma kwa wateja.

Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya CRDB, Frederick Nshekanabo alisema utoaji wa mikopo kidijiti umechangia kwa kiasi kikubwa kurahisisha kufikisha huduma kwa wateja na kukidhi mahitaji yao kwa wakati, hivyo kuipa benki faida hiyo nono huku ikipunguza vihatarishi.

Alisema uwiano wa mikopo isiyolipika umepungua na kufika asilimia 2.8, chini ya wastani wa soko kwa sasa ambao ni asilimia 35 na kukidhi masharti ya kikanuni yanayotaka usizidi asilimia tano. Jumla ya mikopo ghafi iliyotolewa katika kipindi hicho ni Sh. trilioni 7.2, sawa na ongezeko la asilimia 4.6 kulinganishwa na Sh. trilioni 6.9 zilizokopeshwa mpaka Desemba 31, 2022.

Benki ya CRDB imewekeza zaidi kwenye teknolojia ili kuwaruhusu wateja kutumia huduma zake mahali popote walipo na kwa urahisi kukamilisha malengo yao.

Vilevile, benki hiyo inachukua hatua muhimu kuhakikisha inakuza mizania yake kwa kuboresha huduma na kukidhi mahitaji ya wateja. Katika robo hii ya kwanza, mali za benki ziliongezeka kwa asilimia 9.3 na kufika Sh. trilioni 11.96 kutoka Sh. trilionio 11.69 zilizokuwapo mpaka Desemba 2022, huku amana za wateja nazo zikipanda kwa asilimia 1.3 na kufika Sh. trilioni 8.3 kutoka Sh. trilioni 8.2 zilizokuwapo Desemba 2022.

Nsekela alisema kesho ya benki ina matumaini zaidi kwa kuwa kwa miaka mitano iliyopita ilikuwa na changamoto nyingi ambazo menejimenti ilijitahidi kukabiliana nazo.

Kutokana na mikakati inayofanya kuwahudumia wafanyabiashara wadogo na wa kati, Benki ya CRDB imetunukiwa zawadi ya Benki Bora kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati kwa mwaka 2023 na Taasisi ya Global Finance ya Uingereza. Tuzo hiyo ilitolewa katika robo hii ya kwanza.

# Hoja ya ukata ilivyoteka kampeni uchaguzi TLS

**Na Elizabeth Zaya**

WAGOMBEA wa nafasi ya urais wa mwaka 2023/24 wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) jana walichuana kunadi sera zilizotekwa na hoja ya kukikomboa chama hicho kutoka katika ukata kiuchumi unaokikabili kwa sasa.

Wagombea wa nafasi hiyo ni Anold Sungusia na Reginald Shirima. Kila mmoja alitoa ahadi hiyo ya kukinasua chama hicho wakati akinadi sera zake kwenye mdahalo ulioandaliwa na TLS mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza katika mdahalo huo baada ya kuulizwa mipango aliyonayo kwa chama hicho, Sungusia alisema TLS kuwa hoi kiuchumi ni jambo la aibu.

"Ninakubali kwamba TLS kwa sasa ina hali mbaya kiuchumi. Hii ni aibu. Hatupaswi kuwa hivi. Chama chetu kuwa hoi kifedha ni kituko, ni aibu kubwa kwetu," alisema Sungusia.

Aliahidi kuwa akichaguliwa kuwa rais wa chama hicho, lazima aweke misingi na miongozo imara itakayosaidia kukipatia fedha za kujiendesha bila mkwamo ikiwamo kuwa na miradi mbalimbali ya uzalishaji kiuchumi.

Pia alisema ataweka misingi ya kupambana na maadui sita ambao wamechangia kwa kiwango chama chao kuwa na hali mbaya kiuchumi. Aliwataja ni kukosa umakini, uvivu, kuchukulia mambo kawaida, tabia ya kupenda kujitetea, uoga wa kuthubutu kufanya mambo, na kufanya vitu vya kujifurahisha ambavyo havileti fedha.

"Kwa hiyo wakinichagua, nitakachokifanya cha kwanza ni kutengeneza sera ambayo itapambana na hao maadui sita pamoja na kuwatengenezea mawakili uhakika wa kufanya shughuli zao bila bughuza na kujipatia kipato chao. Na hiyo haihitaji miaka mingi ni kuweka tu misingi," alisema Sungusia.

Mgombea mwingine wa nafasi hiyo, Shirima, alisema miongoni mwa mambo atakayoyashughulikia ya kusaidia kuinua TLS ni kutafuta vyanzo vya mapato kujazia pale chama hicho kilipopungiwa.

Pia alisema atazungumza na serikali ili isaidie kuipatia fedha TLS kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali za chama hicho.

Uchaguzi wa viongozi wa TLS unatarajiwa kufanyika mwezi huu jijini Arusha kumpata atakayechukua mikoba ya Prof. Edward Hoseah anayemaliza muda wake katika nafasi hiyo ya urais.

Viongozi wengine wanaotarajiwa kuchaguliwa katika uchaguzi huo ni nafasi ya makamu wa rais, viongozi wa kanda na viongozi wa mawakili vijana.

# Uhakiki leseni udereva wakwaa kigingi, polisi wabaini udanganyifu

## •LATRA yaongeza muda

**Na Elizabeth Zaya**

MAMALAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) imeongeza muda wa miezi mitatu wa kuthibitisha na kuwasajili madereva.

Wakati LATRA ikifanya hivyo, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nalo limeongeza muda wa ukaguzi wa leseni.

Kwa mujibu wa LATRA, uamuzi huo umetokana na idadi ndogo ya madereva waliojitokeza kujisajili na ukaguzi wa leseni zao. Mwisho wa usajili na ukaguzi za leseni kwa madereva hao ulikuwa Aprili 30 mwaka huu.

Machi mwaka huu, Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillus Wambura alitoa maagizo kwa wakuu wa vikosi vya usalama barabarani vya mikoa kufanya ukaguzi na uhakiki wa shule zote za udereva nchini ili kujua kama zinakidhi ubora.

Agizo hilo lilitolewa baada ya Jeshi la Polisi kugundua mfumo mbovu wa upatikanaji wa madereva kuwa ni chanzo kingine cha ajali nchini zinazogharimu maisha ya wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi jioni, Kamanda Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhani Ng'anzi alisema hadi kufikia Aprili 30, jumla ya leseni za madereva 20,944 sawa na asilimia 1.2 pekee ndio zilizohakikiwa.

Alisema leseni za madereva 17,726 zimebainika kuwa na sifa na kupewa barua ya uthibitisho, huku leseni 3,214 zikifutiwa madaraja kutokuwa na sifa ya daraja C na E, kwa kutosomea madaraja hayo.

"Tanzania tunao madereva wa mabasi na malori zaidi ya milioni mbili, hadi sasa waliohakikiwa keseni zao haijafika asilimia mbili," alisema.

"Nitoe ufafanuzi kwa madereva wote nchini kuwa na ukaguzi wa shule au vyuo vinavyotoa mafunzo ya udereva na uhakiki wa leseni, sio wa kumkomoa dereva au kampuni mojawapo, lengo ni kujua madereva wanaoendesha magari barabarani, kama wana sifa au wanamiliki leseni kihalali na walizipata kwa kufuata utaatibu," alisema Kamanda Ng'anzi.

Kuhusu uhakiki wa shule na vyuo vya udereva, Ng'anzi alisema kuwa jumla ya shule na vyuo 297 vilivyohakikiwa, 134 pekee ndivyo vyenye sifa, na 161 vilifungwa kutoa mafunzo kutokana na kukosa sifa na kukidhi vigezo.

"Vyuo na shule hizi zimefungwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutokuwa na madarasa badala yake wamekuwa wanatolea mafunzo kwenye flemu, kuwa na magari mabovu na kutofuta mtaala," alisema.

Akizungumzia ukaguzi wa madereva na kuwathibitisha, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Barabara wa LATRA, Johansen Kahatano alisema wameamua kuongeza miezi mitatu kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza.

Alisema hadi kufikia Aprili 30, jumla ya madereva 3,334 ndio waliokaguliwa na kuthibitishwa, idadi aliyoitaja ni ndogo.

"Tumegundua madereva wengi hawana vyeti, lakini kuna urasimu kwenye kupima afya kutokana na gharama, suala la afya tumeliondoa tutalifanya baadaye, hivyo tutaongeza muda wa miezi mitatu hadi Julai 31," alisema Kahatano.

Alisema lengo sio kuwakomoa, bali watambue kinachofanyika endapo wanataka kuifanya kazi ya udereva ili itambulike kama taaluma nyingine.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Madereva Tanzania (TDF), Jackson Ruhahas, alisema Tanzania ina zaidi ya leseni milioni nne na kwamba kuhakiki kwa mwezi mmoja ni kitu kisichowezekana.

Alisema mifumo ya LATRA na Jeshi la Polisi ni haifanyi kazi kwa ufanisi; na wakaguzi wenyewe ni wachache.

## Mvua yaua bibi na wajukuu

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU watatu, bibi na wajukuu zake wawili, wakazi wa Mtaa wa Bomani katika Halmashauri ya Mji Tarime, wamefariki dunia baada ya kusombwa na maji ya mvua iliyonyesha Jumapili jioni.

Waliofariki ni Ghati Magabe (60), Johnson Daniel (10) na Vailent Daniel (3) huku mama watoto wa watoto hao wawili, Neema Daniel akinusurika baada ya kushika mti na kuomba msaada.

Mbali na vifo hivyo, mvua hiyo pia imesababisha mabwawa matatu na vizimba vya samaki kubomoka na hivyo wafugaji samaki kupata hasara.

Katika Hospitali ya Wilaya Tarime mjini hapa jana, mume wa Ghati, aliyejitambulisha kwa jina Magabe na mjukuu wake, Joseph Robhi, walisema familia yao imepata pigo kubwa kutokana na vifo hivyo.

"Mimi nina familia nyingine, tunaishi Kijiji cha Kewamamba, tulipa taarifa ya Ghati na wajukuu wetu hao wawili wamesombwa na maji ya mvua iliyonyesha na kusababisha Mto Bomani kujaa na maji kubomoa mabwawa ya samaki na mengine kukumba nyumba walimokuwa wanaishi na wajukuu zake hao na binti yetu, mama wa watoto hao (Neema) aliyenusurika baada ya kung'ang'ania kwenye mlingoti uliokuwa ndani ya nyumba huku akipiga kelele za kuomba msaada wa kuokolewa.

"Tulifika na kuwakuta wananchi, polisi na askari wa

Zimamoto na Uokoaji wakiwa wanafuatilia kuwatafuta hao ndugu zetu waliosombwa na maji. Mtoto mmoja, Johnson alipatikana akiwa amefariki dunia.

"Tuliendelea kuwatafuta wengine na leo (jana) tumefanikiwa kuikuta miili ya Ghati na Vailent ikiwa pembeni mwa mto huo wakiwa wamefariki. Miili hiyo ipo hapa Hospitali ya Wilaya na tumeitambua kuwa ni ya Ghati na wajukuu zake wawili, Johnson na Vailent," alisema Magabe.

Mmiliki wa Chuo cha Ufundi na Radio Sachita wilayani Tarime, Peter Mwera alisema: "Mvua iliyonyesha Jumapili jioni imeleta madhara makubwa kwetu na jamii ikiwamo kusombwa mabwawa, vizimba vyetu vitatu vya samaki, ukuta kubomoka na kusababisha samaki kusombwa na maji."




Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, akiongea na wafanyakazi wa Barrick wakati alipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye maonesho ya OSHA mjini Morogoro jana ambapo alifurahia teknolojia mbalimbali za usalama zinazotumiwa na kampuni kuhakikisha usalama mahali pa kazi pia alipongeza kampuni kushinda tuzo ya jumla katika maonesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utouh amsifu mkulima kushtaki aliowataja CAG

**Na Jenifer Gilla**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, amesifu uamuzi aliouchukua mkulima Thomas Nkola, kuamua kufungua kesi mahakamani kushinikiza waliotajwa kuhusika na ubadhirifu wa mabilioni katika ripoti ya mwaka 2021/22 ya CAG kuchukuliwa hatua.

Nkola, mkulima na mkazi wa Mtaa wa Majengo wilayani Maswa mkoani Simiyu, ameamua kufungua kesi hiyo kwa kuzingatia Ibara ya 27(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Ibara ya 27(1) inatamka: "Kila mtu ana wajibu wa kulinda mali asilia ya Jamhuri ya Muungano, mali ya Mamlaka ya Nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine."

Ibara ya 27(2) inatamka: "Watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhilifu, na kuendesha uchumi wa taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya taifa lao."

Katika mazungumzo na Nipashe jana, Utouh aliyekuwa CAG kwa miaka minane kuanzia mwaka 2006 hadi 2014, aliutaja uamuzi wa mkulima huyo kuwa ni wa kihistoria na mfano wa kuigwa.

Alisema mwananchi huyo wa kawaida anafanya jambo la maana lililopaswa kufanywa na viongozi husika. Alisema mkulima huyo ametuma ujumbe kwa serikali na watekelezaji wa sera na sheria kwamba wananchi wamechoshwa na vitendo vya ubadhirifu vinavyojitokeza kila mwaka na havichukuliwi hatua stahiki za kuvikomesha.

Alisema kitendo hicho kinapaswa kifungua akili za wadau ikiwamo wanasheria. Aliwataka wasome Katiba na Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kutumia utaalamu wao kuchanganua kitu hicho alichokifikiria mwananchi wa kawaida.

Hata hivyo, Utouh ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, alisema changamoto atakayokutana nayo mkulima huyo katika kesi hiyo, ni kukosa ushahidi uliojitosheleza ikiwa atategemea kutumia nyaraka za ripoti ya CAG kama ushahidi wa kupeleka mahakamani waliotajwa.

"Lakini, kwa kuwa ni kitu ambacho kimetokea kwa mara ya kwanza, kinaweza ishangaza mahakama. Kama mtu wa kawaida anaweza kujipanga mpaka apate mawakili, kwanza ni gharama.

"Inaonyesha amedhamiria na anajua nini anataka kufanya. Kwa hiyo, matokeo yoyote atakayopata bado itabaki kuwa ni tukio la kihistoria," alisema

Utouh alisema majibu yatakayotokana na kesi hiyo pia yatakuwa somo kwa wakaguzi na wadhibiti wa hesabu; na vyombo vya usalama kufanya majukumu yao ipasavyo ili kuzuia kuendelea kwa ubadhirifu wa fedha za umma na kuitia serikali hasara huku wananchi wakiteseka na umasikini.

Utouh alisema kuwa ili Tanzania ipate maendeleo na kuepukana na vitendo vya ubadhirifu, viongozi wapewe majukumu kulingana na utaalamu na uzoefu walionao katika nafasi hiyo.

Kwa mashirika ya umma yanayoendeshwa kibiashara, Utouh alishauri viongozi wake wasipatikane kwa kuteuliwa, bali nafasi hizo ziwe zinatangazwa na kuombwa na watu ambao watafanyiwa usaili.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ombi la wafanyakazi kuboreshewa sheria za kazi lifikiriwe

**WAKATI** jana dunia ikiadhimisha Siku ya Wafanyakazi iliyokuwa na kaulimbiu 'Mishahara Bora na Ajira za staha ni Nguzo ya Maendeleo kwa Wafanyakazi' ni muhimu maombi yao yakasikilizwa na kufanyiwa kazi.

Katika baadhi ya maombi yao ni pamoja na serikali kuongeza motisha kwa wafanyakazi kwa kuwawekea mazingira mazuri, kuwasikiliza na kutekeleza makubaliano kwa mujibu wa sheria na mkataba wa kazi.

Kilio cha wafanyakazi wanaofanya sekta ya elimu ni kuishi katika mazingira duni na wanachohitaji ni motisha ya mishahara na kuwaboreshea mazingira ya ufanyaji kazi wao.

Pia, kuna haja ya serikali kuboresha sheria ya kazi ili kumlinda mfanyakazi hasa katika suala la mikataba ya kazi iwapo atasitishiwa mkataba wake alipwe stahiki zake kwa wakati.

Wakitoa malalamiko yao baadhi ya wafanyakazi walidai kuwa serikali inaweza kuvunja makubaliano yalioko kwenye mkataba na mfanyakazi wake, lakini hakuna hatua itakayochukuliwa. Kwa mfano mfanyakazi ana haki ya kupata nyongeza ya mshahara kila mwaka unavyoanza, maana yake inavyofika Julai mosi, wanategemea mfanyakazi huyo aanze kuona nyongeza ya mshahara.

Pia, mfanyakazi anapotenda kosa, anahukumiwa kwa mujibu wa sheria na mkataba alioingia, lakini serikali inapokiuka mkataba huo hakuna kinachoamuliwa na mtu anapokosa anaweza fukuzwa kazi au kuishia kwenye mazingira magumu.

Kadhalika suala la nyongeza ya mishahara limekuwa kama hisani kutokana na kutangazwa, lakini utekelezaji wake unachukua muda mrefu.

Wafanyakazi wa sekta ya elimu wamedai, kuna mambo makuu matatu ambayo ni mazingira, mtaala, na washikadau, ambavyo vikiweza kufanyika kwa ufanisi nchi itapata kusudio halisi la taifa kwenye elimu.

Kwa upande wa sekta ya afya, nao wameomba madaktari kukumbukwa hasa walioko vijijini ambao imedaiwa wanafanya kazi katika mazingira magumu ikiwamo kuishi kwenye nyumba zenye ubora hafifu.

Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), limesema malalamiko makubwa ya wafanyakazi wengi nchini ni kutaka kupewa mishahara bora na ajira zenye staha.

Kadhalika, wafanyakazi wengi kufanyishwa kazi bila mikataba hali inayowafanya washindwe kupata haki zao na wengine hata kudhulumiwa pale inapotokea shida na mwajiri wake.

Chama hicho kimedai kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi kwenye taasisi mbalimbali na sekta binafsi wakitumikishwa kwa muda mrefu bila kupewa mkataba jambo ambalo liko kinyume cha sheria.

Pia, chama hicho kimewataka waajiri nchini kujali maslahi ya wafanyakazi na kufuata makubaliano kwa mujibu wa mikataba waliyokubaliana, kutowanyanyasa wafanyakazi na kuwalipa fedha za kufanya kazi nje ya muda.

Shirika la Kazi Duniani (ILO), pia limetaja njia bora za kufanyika ili kutoa kazi bora, kukabiliana na ukosefu wa usawa kazini na kupunguza umaskini kwa jamii ili ijikimu na kujenga maisha yao ya baadaye.

Ujumbe uliotolewa na Mkurugenzi wa Shirika hilo, Gilbert Houngbo, umetaja njia hizo kuwa ni kufanyika mabadiliko ya kimuundo ya muda mrefu ikiwamo kubuni teknolojia mpya itakayosaidia kuongeza ajira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Pia, sera na matendo lazima yazingatie ubinadamu, ili kuruhusu watu kufuatilia ustawi na maendeleo yao ya kiroho katika hali ya uhuru na heshima, usalama wa kiuchumi na fursa sawa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hoja ujenzi sanamu ya Nyerere makao makuu ya AU ina mashiko

**KATIKA** kuenzi juhudi za Hayati Mwalimu Nyerere, serikali ya Tanzania ikatumia mkutano wa Jumuiya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), ambao unaofanyika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kukumbusha ujenzi wa sanamu yake kwenye makao makuu ya Umoja wa Afrika (AU).

Mwakilishi kwenye mkutano huo kutoka Tanzania, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Shabani, akaahidi ujenzi wa sanamu la Nyerere ni miongoni mwa hoja atakazowasilisha kwenye mkutano huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, alitoa kauli hiyo kwenye ufunguzi wa mkutano wa Kamati ya Kudumu ya Makatibu Wakuu wa SADC, uliofanyika huko nchini DRC.

Akasema pamoja na kujadili kuhusu sanamu hilo, pia watakumbushia Tafsiri ya Nyaraka muhimu za SADC, kuwekwa katika lugha ya Kiswahili ambayo ni hatua muhimu ya utekelezaji wa matumizi ya lugha ya hiyo kwenye Jumuiya.

Mengine ni Mpango wa Kanda wa Ununuzi wa Pamoja wa Bidhaa za Afya unaoratibiwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na mkakati wa pamoja wa Kanda wa Kusimamia Sekta ya Mbolea.

Mwenyekiti wa Mkutano huo ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mtangamano wa Kikanda wa DRC, Balozi Songhu Kayumba, aliwasihi wajumbe kushiriki kikamilifu kwa kutoa maoni yatakayolenga kufanikisha utekelezaji wa agenda zitakazojadiliwa.

Alisema, makatibu wakuu na wajumbe watajadili ajenda mbalimbali, ambazo ni pamoja na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maamuzi ya wakuu wa nchi na serikali, waliyotoa katika mikutano iliyopita.

Ni fahari tunayopaswa kujivunia kama Watanzania, pale taifa linapoamua kuunga mkono juhudi za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwenye kupigania uhuru wa taifa hili na mengineyo jirani.

**Nikirejea kile Tanzania inadai kuanzia na jukwa la SADC, Nyerere yumo katika kundi la waasisi waliohangaikia kuasisiwa kwa chombo hicho, kikiwa na umri wa miaka 60, kizazi cha sasa tukifaidi matunda yake.**

Kwa kuwa mikutano hii huhudhuriwa na viongozi wakubwa kutoka nchi mbalimbali, jambo hilo litaiongezea heshima hadhi ya lugha yetu kwenye maeneo tofauti tofauti ya nchi.

Pia, litaongeza ajira kwa wasomi wa lugha hiyo, kwa kuwa watu kutoka mataifa mbalimbali watataka kujifunza kama ilivyo kwa sasa, mataifa mengi yana shauku ya kuijua.

Katika maisha ya kawaida na historia zaidi ya nchini na bara Afrika, Nyerere anabaki kioo na mtu aliyefanya makubwa ya kihistoria kwa Waafrika wenzake watafutao haki zao, katika pande mbalimbali.

Haishiii katika nchi za Afrika Mashariki na kato pekee, Nyerere hakujenga wazo la kutaka kuona jirani yake anaatabika mbele yake. Hata imefika hatia nchi za Kusini mwa Afrika, ni ngumu sana kuzungumzia uhuru wao, bila kumtaja Nyerere na Tanzania yake kwa namna moja na nyingine.

Miji ka Mpwapwa imebaki kuna na nyayo za weakati kutoka ukanda huo, mataifa ya Namibia, Angola na Afrika Kusini iliyoelemewa na lindi ya ubaguzi dhidi yao, huku Msumbiji nayo ina kila sura ya msaada wa Nyerere, hata mpaka leo inabak8i kuwa rafiki kiopenzi wa taifa hili.

Nikirejea kile Tanzania inadai kuanzia na jukwa la SADC, Nyerere yumo katika kundi la waasisi waliohangaikia kuasisiwa kwa chombo hicho, kikiwa na umri wa miaka 60, kizazi cha sasa tukifaidi matunda yake.

Katika hilo binafsi katika mawazo yangu, naamini ni haki na sawa kabisa kukubaliana hatua ya muasisi huyo wa taifa letu, akiwa na rekodi ya wema kimataifa barani Afrika aenziwe kama tunavyofanya sisi, ikiwa ni ishara ya shukurani na utambulisho wake kimataifa.

# Ndoto ya Samia kuifufua NARCO yaanza kutimia

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeiwezesha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) Sh. bilioni 4.65 kununua vitendea kazi na ng'ombe wazazi ili kuboresha na kuongeza uzalishaji wa kampuni hiyo.

Hayo yamefahamika wakati wa ziara ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyoifanya katika Ranchi ya Kongwa wilayani Kongwa jijini Dodoma mwishoni mwa wiki.

Wakati akizindua matreka mapya matano na kupokea ngo'mbe 1,000 kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa kampuni ya NARCO, Ulega alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha kampuni hiyo iweze kujiendesha kibiashara.

Alisema lengo la Rais Samia ni kuiimarisha NARCO kwa kuboresha miundombinu na vitendea kazi ili waweze kunenepesha ng'ombe, kuimarisha biashara ya nyama bora ya Kongwana kuzalisha malisho ya mifugo kwa wingi kwa ajili ya kuyauza ndani na nje ya nchi.

"Hivi sasa tumeshafika katika kiwango cha kuuza nje ya nchi nyama tani 12,000 na kuanzia mwaka ujao na kuendelea tutatoka kwenye tani hizo na kutafuta tani 50,000 na ikiwezekana mpaka tani 100,000," alisema.

Pia, alisema katika mkakati wa kuifufua kampuni ya NARCO wataanzisha skimu za unenepeshaji wa mifugo ili nyama itakayokuwa inazalishwa kutoka NARCO iwe na ubora wa kuiuza nje ya nchi.

"Tunakusudia kwamba mchango wa sekta ya mifugo uongezeke kutoka asilimia saba hadi kufikia asilimia zaidi ya 10, na hilo linawezekana kwa sababu rasilimali ya kutuwezesha kufikia huko tunayo," alisisitiza.

Alisema, serikali ina mipango ya kuanzisha skimu za umwagiliaji wa malisho ili yaweze kuzalisha kwa wingi kwa ajili ya kuyauza ndani na nje ya nchi.

"Kama tunavyosafirisha mahindi kutoka maeneo mbalimbali na kuwapelekea wahitaji tunataka pia tuzalishe malisho kwa wingi na kuyasafirisha kuyapeleka kwa wahitaji waliopo ndani na nje ya nchi," alifafanua.




Ofisa Mkuu Utawala wa NSSF, Daniel Shaidi (kushoto) akimkabidhi mfuko mwanachama mstaafu, mzee Anselmi Fungosita, baada ya kutembelea banda lao wakati wa Maonesho ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) yaliyofanyika viwanja vya Tumbaku Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mstaafu: Bila NSSF ningeadhirika

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

MWANACHAMA mstaafu wa NSSF, Anselmi Fungosita, ameushukuru Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa kuendelea kumlipa pensheni yake ya uzee kila mwezi kwa kipindi cha miaka 14 bila ya kupata usumbufu na kuendelea kuishi maisha mazuri.

Fungosita alibainisha hayo mjini Morogoro, wakati alipotembelea banda la NSSF katika Maonesho ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), yanayoendelea katika viwanja vya Tumbaku.

"Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa uhai huu na kuifanya Serikali yetu ya Tanzania kuweka mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii kama NSSF, kwa sababu mimi nimestaafu miaka kumi nne iliyopita na nilivyoenda katika ofisi za NSSF nilikutana na wafanyakazi ambao walinishauri vizuri, waliniambia baba usichukue fedha zako zote chukua kiasi fulani na kilichobaki utakuwa unapokea pensheni ya uzee kila mwezi. Nilikubali ndio maana mpaka leo hii nina faidi matunda kwa kupata malipo yangu ya pensheni kila mwezi ambayo yana nisaidia kupata mahitaji yangu," alisema Fungosita. Aidha, alipongeza Mfuko kwa kuyafikia makundi mbalimbali ya wajasiriamali na kuwapa elimu ili waweze kujiunga na kuchangia kwa ajili ya maisha yao baadaye.

"NSSF mmefanya kitu kizuri sana ninawapongeza kwa kutoa fursa kwa watu waliojiajiri wenyewe ili waweze kunufaika na hifadhi ya jamii ikiwemo mafao ya uzee," amesema.

Alisema, bila ya pensheni anayolipwa na Mfuko maisha yake yangekuwa magumu hasa ikizingatiwa kuwa hana nguvu za uzalishaji mali.

Katika hatua nyingine, Fungosita amesema kuwa NSSF inampa fursa mbalimbali ikiwamo kupata mkopo benki kupitia pensheni yake.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Kumekucha fidia Mradi wa Kabanga

**Na Mwandishi Wetu,**
NGARA

MKUU wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Kahabi, ametia saini majedwali ya fidia ya Mradi wa Kabanga Nickel unaoendeshwa na Kampuni ya Tembo Nickel, hatua inayotoa fursa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kuyapitia majedwali na kuyaidhinisha kwa lengo la kuiruhusu kampuni kulipa fidia stahiki kwa wanaoguswa na mradi.

Akizungumza baada ya kutia saini majedwali hayo, Kanali Kahabi alisema anafarijika kuona shughuli za uthamini zimekamilika na sasa zimebaki hatua chache kabla ya wananchi kulipwa fedha zao na mradi uanze shughuli zake.

"Hatua hii ilikuwa inasubiriwa kwa hamu kubwa, si tu kwa wananchi wanaoguswa na mradi huu, bali pia kwa wanangara nzima. "Tunaamini Kampuni ya Tembo Nickel ambayo ndiyo inaendesha huu mradi itakapoanza shughuli zake, itakuwa na mchango mkubwa kwa maisha ya wananchi wetu na taifa kwa ujumla.

"Kwa hiyo, leo kuona wananiletea haya majedwali nitie saini, inamaanisha kweli sasa mambo yameiva, tunakaa mkao wa kuanza kuona shughuli za mradi zinaanza, watu waone matunda yenyewe sasa.

"Kikubwa, nimshukuru sana Meneja Mkazi wa Kampuni ya Tembo Nickel, Benedict Busunzu, na timu yake. Wameonyesha kweli wako makini na wanataka mradi huu uanze kama ilivyo nia ya Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye anataka mgodi huu uanze ili wananchi wanufaike na taifa pia lipate mapato," alisema Kanali Kahabi.

Alisema kuwa baada ya kutia saini majedwali hayo, kwa sasa anawataka wananchi wanaoguswa takribani 1,300 wanaotarajiwa kupisha mradi huo, kuwa na subra na kumpa Mthamini Mkuu wa Serikali muda wa kuyapitia na kuyaidhinisha ili kila anayeguswa, alipwe fidia stahili na kupisha shughuli za mradi.

"Lengo la serikali ni kuona kila mwananchi analipwa kile anachostahili kabla ya kuachia ardhi yake kuchukuliwa na mradi. Pia tunafahamu kuwa uchimbaji wa madini ya nikeli ukianza hautonufaisha tu wananchi wa Ngara, bali taifa zima.

"Huu ni mradi mkubwa na wa kimkakati ambao tunatarajia utainua uchumi wa nchi hii, ndiyo maana Mheshimiwa Waziri wa Madini, (Dk. Doto Biteko) na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, walikuwa wanafuatilia kwa ukaribu uthamini ulipokuwa unaendelea na kwa kweli viongozi hawa wametupa ushirikiano wa kutosha na kutuongoza hadi leo hii ninapotia saini majedwali haya," alisema.

Msimamizi Mshauri wa Mkandarasi Elekezi, Basil Shio, kutoka Kampuni ya RSK, alisema kabla ya Mkuu wa Wilaya, Kanali Kahabi, kutia saini majedwali hayo, kulikuwa na hatua mbalimbali za uthamini ambazo zimefuatwa kama sheria inavyotaka ikiwamo kuwaonyesha wanaoguswa fidia zao stahili na kupata idhini yao.

Shio pia alisema kabla ya ulipaji wa fidia wanaoguswa wote watapewa elimu ya matumizi ya fedha na baadaye kufunguliwa akaunti maalum hususani akaunti ya pamoja kwa wenye wenza ambayo ndiyo itakayotumika kulipa fidia hizo.

"Tunajua kuwa watu wana akaunti za benki, lakini lengo letu sisi mtu kama alipaswa kulipwa kiasi fulani cha fedha, tunataka zile fedha zote zimfikie, ndiyo maana tunafungua akaunti maalum ambazo mwananchi hatolipa makato yoyote yale, kama mtu una mwenza wako itafunguliwa akaunti ya pamoja," alisema Shio.

Wathamini wa Mradi walianza shughuli za uwandani Julai mwaka 2022. Walitambua na kupima eneo lote la mradi na kutambua wanaoguswa, kuandaa majedwali ya fidia kisha kuyaweka wazi kwa waguswa kwa kuzingatia misingi ya sheria kabla ya majedwali kuidhinishwa na watendaji wa vijiji na kata husika, Mthamini wa Mkoa na Ofisa Ardhi Mteule wa Wilaya.



Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Kahabi, akitia saini majedwali ya fidia ya Mradi wa Kabanga Nickel unaoendeshwa na Kampuni ya Tembo Nickel, ikiwa ni ishara ya kutoa fursa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kuyapitia na kutia saini ili kampuni ilipe wananchi fidia kabla ya kupisha shughuli za mradi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## GGML kinara wa kuzingatia SDG

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited (GGML) imeibuka mshindi wa jumla katika tuzo za kampuni za kibiashara zilizoonyesha kwa vitendo mchango wake kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) kwenye kipengele cha kujali watu.

Tuzo hiyo iliyotolewa na Shirika la UN Global Compact Network Tanzania mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, imetajwa kuthibitisha nia ya GGML kujitolea kuisaidia jamii inayozunguka mgodi huo.

Pia imetajwa kuthibitisha nia ya kampuni hiyo kuimarisha mazingira mahali pa kazi kuwa salama na shirikishi huku wafanyakazi wake wakitekeleza majukumu yao kwa kuzingatia utu.

Akipokea tuzo hiyo, Mkurugenzi wa Bodi ya GGML, Felix Mlaki alisema: "Tuzo hii ni ushuhuda wa dhamira yetu ya kusaidia jamii inayozunguka mgodi wetu pamoja na juhudi zetu za kuwa na mahali pa kazi panapozingatia afya na usalama kwa wafanyakazi wetu."

Alisema kuwa baada ya kupata tuzo, kampuni hiyo itaendelea kuimarisha dhamira yake kama sehemu ya Uwajibika wa Kampuni kwa Kijamii (CSR) kwa kutekeleza miradi inayofanana na juhudi za serikali katika kuendeleza jamii.

"Tuzo hii inatambua juhudi zetu za kuheshimu haki za binadamu na uendelevu wa mazingira huku tukishirikiana na jamii kutekeleza miradi mbalimbali kupitia mpango wa uwajibikaji kwa jamii," alisema.

Alibainisha kuwa kampuni itaendelea kuboresha maisha ya makandarasi wa ndani, ikiwa ni pamoja na kuwapa kipaumbele katika fursa za zabuni ili waweze kuchangia upatikanaji wa ajira kwa watanzania wengi katika shughuli za uchimbaji madini.

Tuzo hizo zilizozinduliwa Februari mwaka huu, zinalenga kuendeleza ushirikiano kati ya wadau wa sekta binafsi na serikali katika utekelezaji malengo ya maendeleo endelevu.

# RC amulika rushwa ya ngono kazini

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhakikisha rushwa ya ngono mahali pa kazi inatokomezwa katika mkoa huo.

Akizungumza jana wakati wa sherehe za maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani ambayo kimkoa ilifanyika mjini hapa, Serukamba alisema tatizo la rushwa ya ngono ni lazima likomeshwe Singida.

Serukamba pia aliliagiza Shirika la Bima Mkoa wa Singida kufanya uhakiki wa wafanyakazi ambao bima zao zimeiva ili walipwe; na wakurugenzi wa halmashauri ambao hawawalipi watendaji posho za kila mwezi kuanza kufanya hivyo haraka.

Mratibu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) Mkoa wa Singida, Maria Bange, akisoma risala ya wafanyakazi, alimesema rushwa ya ngono katika harakati za kutafuta ajira imepungua katika kipindi cha 2022/23.

Alisema katika kipindi hicho kumekuwa na changamoto kadhaa ikiwamo baadhi ya viongozi kuwaweka ndani wafanyakazi bila kufuatia utaratibu na sheria za kazi.

Alisema changamoto nyingine ni nyongeza ya mishahara iliyofanyika mwaka jana kutokidhi matarajio ya wafanyakazi, kutolipwa kwa wakati fedha za uhamisho, likizo na malimbikizo ya mishahara, hata baadhi ya watumishi kustaafu na huku malipo ya pesheni zao yakicheleweshwa.

Changamoto nyingine ni Shirika la Bima kutowalipa watumishi waliokata bima ya maisha wakati bima zao zinapoiva, waajiri binafsi kutowasilisha makato ya asilimia 10 kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, waajiri kutopeleka michango ya hifadhi ya jamii kwa wakati na kusababisha tozo kubwa (penalti).

Bange alisema pamoja na changamoto hizo, wafanyakazi wanaomba serikali iongeze nyongeza ya kima cha chini Cha mshahara inayoendana na hali ya uchumi wa sasa, kuhamisha wafanyakazi kuendane na ulipaji wa stahiki zao na madeni ya watumishi yalipwe.

Alisema waajiri wa sekta binafsi watoe mikataba ya kudumu kwa wafanyakazi, likizo na kima cha chini cha mshahara kizingatiwe na sekta binafsi na mabaraza ya wafanyakazi yafanyike kwa wakati, malipo ya posho yatolewe kwa mujibu wa sheria na usiwe hisani ya mwajiri na kodi kwenye mishahara iendelee kupunguzwa.



## BoT yatakiwa kusimamia kanuni kuhudumia wateja

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI imeagiza Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kusimamia kanuni, utaratibu na sheria ili benki zote nchini zifanye kazi zao kwa kuzingatia weledi kuwahudunia wananchi.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati akizindua tawi jipya la benki ya Mwanga Hakika Benki.

Katika hatua nyingine waziri huyo, ameitaka benki hiyo, kujiendesha kwa kutoa huduma nzuri na bora kwa wateja wake.

Pia alitoa rai kwa wateja waliokopa katika taasisi za fedha kurejesha mikopo hiyo kwa wakati ili kuwezesha wengine kukopa kwa kuwa benki zimesaidia ukuaji wa pato la taifa na kwa mtu mmoja mmoja.

"Watu wanaomba fedha kwenye taasisi za kifedha, lakini hawana malengo ninatoa kwa maofisa wote wa benki kuhakikisha kuwa kila mkopaji awe na lengo linaloeleweka ili aweze kurejesha kwa wakati,"alisisitiza Nchemba.

Hata hivyo, Waziri Nchemba, aliwataka wananchi kuwa na nidhamu ya mikopo kwa kuwa watu wengi wanachukua na hawajui chakuifanyia kutokana na kutojiandaa kwa shughuli za kuifanyia.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Mwanga Hakika Benki, Ridhiwan Mringo, alisema benki hiyo, imejipambanua kuwahudumia wateja wengi zaidi, pia itatoa faida kwa wenye hisa na wateja wengine wa benki hiyo.

Alisema benki zimesaidia ukuaji wa uchumi pamoja na kuongeza pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Jagjit Singh, alisema benki hiyo, ilianzishwa mwaka 1998 ikiwa ni ya kijamii na mwaka 2020 ilikuwa ni Microfinance na kuanzia mwaka 2022 mpaka sasa ni benki ya biashara.

Alisema lengo ni kuifanya benki kuwa ya kimataifa zaidi nchini na ifanikiwe kutoa huduma zake ukanda wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kuhudumia watu kwa wingi, pia inatoa riba ya asilimia 12 kwa atayeweka akiba.

# Jumuiya ya wanafunzi mahitaji maalumu yalia na fursa sawa ajira

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JUMUIYA ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), imeanza kupaza sauti, ikiitaka serikali kutafuta 'mwarobaini' wa tatizo la kukosekana kwa ushindani sawa kwenye fursa mbalimbali kwa kundi hilo, hasa ajira na maeneo mengine muhimu.

Aidha, kimeiomba serikali kutatua pia tatizo la upungufu wa vifaa saidizi, unyanyapaa, ukosefu wa fursa sawa za elimu, ajira na maeneo mengine muhimu katika taasisi mbalimbali nchini.

Akizungumza juzi, wakati wa warsha ya kuwajengea uwezo wanafunzi wa MoCU wenye mahitaji maalum, Millu Luhende, ambaye ni mwakilishi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum, alisema matatizo hayo kwa namna fulani yamekuwa yakiwafanya washindwe kujipatia mahitaji fulani ama huduma fulani.

"Kwanza tunaishukuru menejimenti ya MoCU, kwa kuwa kwa mwaka wa masomo 2022/2023, wenye mahitaji maalum tuko jumla ya wanafunzi 35 kutoka idadi ya 29 mwaka wa masomo 2021/2022.

"Idadi hii ilikuwa ndogo zaidi kipindi cha nyuma. Ongezeko hili ni ishara ya jitihada madhubuti za serikali pamoja na chuo chetu kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa na wanafunzi wengine."

Kwa mujibu wa Millu, MoCU kwa sasa ina wanafunzi 15 wenye tatizo la usikivu, lakini kifaa walichopewa na serikali ni kimoja, huku wanafunzi 10 wenye tatizo la viungo, wana viti mwendo vitatu, bajaji mbili.

Katika semina hiyo, Makamu Mkuu wa Chuo cha MoCU, Utawala na Fedha, Prof. Fredy Kilima, alisema menejimenti ya chuo hicho inathamini na kutambua mchango wa watu wenye mahitaji maalum na tayari wanayo sera inayoongoza namna ya kuwatambua na kuwahudumia watu wenye mahitaji maalum.

"Tumekuwa na mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma za watu wenye mahitaji maalum. Tumefanya maboresho kwenye njia nyingi zinazoelekea kwenye huduma muhimu ili watu ambao wanatumia viti mwendo na wenye changamoto za viungo waweze kupita vizuri.

"Kwenye majengo yetu ya zamani tunafanya maboresho kwa mfano sehemu nyingi tumeweka ramps (njia mtelezo) ili wenye viti mwendo waweze kupita bila tatizo. Maktaba yetu, pia tumetoa mlango ambao ni mahusus kupitisha viti mwendo," alisema Prof. Kilima.

Kwa mujibu wa Prof. Kilima, lengo la kuwa na siku hiyo, ni kuwaweka pamoja wenye mahitaji maalum ili kuwatumia wadau kutoa nasaha, kwa maana ya kuwashauri, kuwatia moyo na kuwajenga, licha ya matatizo wanayopitia, bado wanaweza kumudu masomo na kushiriki kwenye fursa mbalimbali.




Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Mwigulu Nchemba kulia akikata utepe kuzindua tawi jipya na la kisasa la benki ya Mwanga Hakika Benki (MHB), jijini Arusha mwishoni mwa wiki.Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Mwanga Hakika, Ridhiwan Mringo **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanasiasa waonywa hujuma eneo la utalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, amewaonya baadhi ya wanasiasa, kuacha tabia ya kuhujumu jitahada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuwaletea maendeleo wananchi wa jiji la Arusha, hasa kwenye eneo la utalii.

Aidha, amekanusha kuwapo mfanyabiashara ndogo ndogo aliyeuawa kama baadhi ya mitandao ya kijamii ilivyoripoti mwishoni mwa wiki.

Mtahengerwa, alisema hayo jana jijini hapa jana wakati akizungumza na Nipashe baada ya taarifa zilizozagaa, kutokana na baadhi ya machinga kuandamana usiku wa kuamkia Aprili 29 eneo la Karakana ya jiji, maarufu kama Depot.

Wafanyabiashara hao, wanadaiwa kulalamikia kunyanyaswa na askari wa jeshi la akiba (mgambo).


Akijibu hoja hiyo, Mkuu huyo wa wilaya alisema; "Hizo ni mbinu zinazotumiwa na baadhi ya wanasiasa wenye nia ovu za kuhujumu na kudidimiza juhudi za Rais Samia katika sekta ya utalii, iliyoongezewa chachu na filamu maarufu ya 'The Royal Tour' ambayo imeongeza idadi kubwa ya watalii nchini.

"Kuna baadhi ya wanasiasa wenye nia ovu ya kuhujumu juhudi za Raisa Samia Suluhu Hassan katika kuwaletea wananchi maendeleo sekta mbalimbali ikwamo ya utalii kwa kutumia machinga kuvuruga amani inayosababisha taharuki kwa umma. Niwaombe waache siasa za maji taka kwa sababu hatutaki kutumia nguvu katika kuwakalibili."

Kuhusu machinga anayedaiwa kuuawa kwa kipigo na askari mgambo, anayetajwa kuwa mkazi wa Kata ya Sombetini, Mtahengerwa, alisema amefuatilia na kubaini kuwa taarifa hizo ni za uongo na uzushi uliojaa uchochezi kwa lengo la kuchafua taswira ya Jiji la Arusha.

"Kamati ya ulinzi na usalama tumefuatilia kwa karibu madai ya machinga kwamba kuna kijana ameuawa. Tumebaini kuwa taarifa hizo ni za uongo na zina lengo la kufanya uchochezi usio na tija yoyote, kwa sababu machinga waliandamana kuelekea Depot ya jiji iliyoko jirani na Kituo cha Afya Ngarenaro, ambako wagonjwa wawili wajawazito walikuwa wanahamishiwa kwenda hospitali ya Rufani Mount Meru.

Mwenyekiti wa Machinga, Mkoa wa Arusha, Amina Njoka, alipoulizwa alisema hakuna machinga yeyote aliyeuawa, taarifa hizo ni za uzushi kwa sababu amezifuatilia kwa kina na hajawahi kusikia machinga anayenyanyaswa na mgambo.



# Watoza ushuru 19 matatani ubadhirifu mamilioni

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, inaendeela na uchunguzi kwa watoza ushuru 19 kutoka Halmashauri ya Wilaya Geita kwa tuhuma za ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 20 baada ya kukiuka kanuni za fedha za serikali kwa kushindwa kuwasilisha benki fedha zilizokusanywa ndani ya saa 24.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Kamanda wa TAKUKURU Mkoa wa Geita, Leonidas Felix, wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi 2023 na kuwa wamefanikiwa kuokoa zaidi ya Sh. milioni 53 zinazotokana na makusanyo ya ushuru wa serikali za mitaa mkoani humo.

Alisema kati ya fedha zilizookolewa Sh. milioni 33 kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'wale ambazo zilipelekwa katika halmashautri hiyo yakiwa ni mapato yanayotokana na makusanyo ya ushuru.

Kadhalika, alisema walifuatilia utekelezaji wa miradi 63 yenye thamani ya Sh. bilioni 11.7 inayotekelezwa katika sekta za elimu, afya, miundombinu ya barabara na maendeleo ya jamii huku wakijiwekea mikakati katika kipindi cha mwaka 2023 ya kuwashirikisha wadau kwa kutoa elimu kwa lengo la kuziba mianya ya rushwa.

"Hali hii inaonesha kuwa vitendo vya ubadhirifu unaoendelea katika katika halmashauri mbalimbali huku akiwaonya watumishi wa umma kufanya kazi kwa uadilifu na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Baadhi ya wananchi mkoani humo wameiomba serikali kuzidisha uchunguzi katika miradi ya serikali kwa kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika kwa lengo la kutoa taarifa za ubadhirifu mapema kabla ya serikali kuingia hasara.



Askofu Dk. Yohana Nzelu akisimikwa kuwa Askofu wa Kanisa la Kiinjili ya Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria inayounganisha Mikoa ya Shinyanga na Simiyu, akichukua nafasi ya Askofu Dk Emmanuel Makala ambaye amestaafu, tukio hilo limefanyika jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Bil. 900/- kuwawezesha vijana kufanya ubunifu

**Na Ibrahimu Mmamba,** SAUT

SERIKALI imeahidi kutoa msaada wa kifedha wa zaidi ya Sh. bilioni 900 kupitia asilimia 10i ya ununuzi ya bajeti ya mwaka 2023 kwaajili ya kuwawezesha vijana kuendeleza ubunifu wao.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Uwezeshwaji Uchumi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Eliakim Mtawa, wakati wa kuhitimisha mafunzo ya uanagenzi kwa vijana 15 yaliyofanyika jijini Mwanza katika Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Alisema serikali inafanya juhudi mbalimbali vijana kuwezeshwa kiujuzi ili wasaidie kusukuma gurudumu la maendeleo kupitia programu mbalimbali ikiwa ni pamoja ya mikopo ya mapato ya ndani ya halmashauri ambayo kwa sasa imesimama kwa muda. "Licha ya mikopo hiyo kusimama kwa muda upo mfuko wa maendeleo ya vijana ambao upo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ulioandaliwa kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35 ambako mkopo huo kwa kiwango cha chini kukopa ni Sh. milioni 50 ambao italipwa kwa miezi 36 kwa riba ya asilima tano kwa mkopo mzima," alisema.

Mtawa aliongeza kuwa serikali imetenga Sh. bilioni 900 kwaajili ya vijana ubunifu na fedha zilizotolewa na serikali kwa vijana hao ni zaidi ya Sh. bilioni 150 ambazo imekuwa ni kinyume na matarajio ya serikali.

Aliwataka wote wanaohitaji mitaji kwa lengo la kuendeleza ubunifu wao kutoa taarifa kwa serikali ili kuona namna ya kufanya waweze kutengeneza mpango kazi wa biashara zao utakao wawezesha kupata mitaji na kuendeleza ubunifu wao.

Meneja wa SIDO mkoani Mwanza, Bakari Songwe alisema tangu kituo kianze kimekuwa na programu mbili za kuhatamia mawazo ya vijana ambako baada ya kukamilisha programu ya uhatamishaji wanatarajia kutengeneza mpango wa kibiashara.

Faustin Mellita, mnufaika wa mafunzo hayo, alisema atajikwamua kutoka kuwa mjasiriamali mdogo hadi kuwa mfanyabiashara na mbunifu mkubwa na matarajio yake ni kujiajiri baada ya mafunzo hayo.

# Wamachinga kujengewa ofisi Kagera

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JUMLA ya Sh. milioni 35 zinatarajiwa kutumika katika ujenzi wa jengo la ofisi ya wajasiriamali maarufu kama Machinga mkoani Kagera kuwawezesha kuendesha shughuli zao na utunzaji wa kumbukumbu.

Akizungumza juzi na Umoja wa wamachinga Mkoa wa Kagera, Katibu Tawala wa mkoa huo, Toba Nguvila, alisema fedha hiyo ni sehemu ya Sh. milioni 10 iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan ikiwa ni ahadi ya kuboresha mazingira ya wamachinga nchini.

"Katika ujenzi wa ofisi hiyo itatumika Sh. milioni 10 iliyotolewa na Rais Samia pamoja na Sh. milioni 25 ambayo itatoka katika Halmashauri za Wilaya kuongeza na kufikia kiwango Sh. milioni 35 ambako ujenzi utaanza mwezi Mei, mwaka huu," alisema Nguvila.

Alisema fedha hiyo ilitakiwa kwenda moja kwa moja kwa wamachinga, lakini uongozi wa mkoa huo ukaona uweke jengo la ofisi ambalo watakuwa huru kupanga shughuli zao na kuweka mkazo katika kazi kwa kuwa wataweka kumbukumbu na sheria za kuwasimamia.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Wamachinga Taifa (SHIUMA), Erenest Masanja alisema, wanatambua nguvu ya serikali kwa kuchangia upatikanaji wa ofisi ambayo itawaunganisha wamachinga wa mkoa huo na kuwa na kauli moja katika kukuza uchumi.

Pia, kupata ofisi, mkoa huo una machinga zaidi ya 100,000 ambao wanakabiliwa na matatizo ya upatikanaji maeneo ya kufanyia kazi, katika kila wilaya na kuiomba serikali kuona umuhimu wa kutatua adha hiyo kwa kuwapa uhuru wa kufanya shughuli zao.

Watumia pikipiki waingiziwa darasa la kiufundi kufikia ufanisi kutumia



Ukurasa 14

Nipashe
TESA
Jumanne Mei 2, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 13

NYAYO ZA MEI MOSI NA KUSHUKA ELIMU...

**Wenye fani wafungua kinachowasibu darasani**

ELIMU
NA HALFANI CHUSI

# Mwanafunzi asiyesikia awapiku wazima kwenye mtihani, akilenga kuwa daktari

• Adokeza ana ndugu kama yeye yuko Chuo Kikuu

KUNAPOZUNGUMZIWA suala la haki sawa kwa jamii ya wenye ulemavu, kuna maana kubwa katika jamii. Ni tafsiri pia, inayobeba maana kubwa kwa watoto wanaosoma shuleni. Mara zote hutajwa, kila anapowezeshwa huwa hashindwi.

Ndiyo inayosogeza udadisi wa Nipashe katika maisha ya kijana Abdul -Azizi Khamis Ali (18), mwenye ulemavu wa uziwi, ambaye licha ya hali hiyo, sasa anaingia katika orodha ya vinara waliofanya vizuri shuleni kwake.

Shule ya Sekondari ya Dk John Joseph Magufuli, alikohitimu Abdul, wamekuwa jumla 103, katika matokeo ya elimu kidato cha nne, imemtoa mwanafunzi mmoja mwenye ufaulu daraja la kwanza, kijana huyo akiwamo, katika orodha watahiniwa tisa waliopata daraja la pili, sita wenye daraja la tatu 28, daraja la nne 59 na sita daraja sifuri.

Akizungumza na Nipashe nyumbani kwao Mwanakwerekwe mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Abdul anasema hakutarajia ngazi hiyo ya ufaulu, kwani alilenga daraja la kwanza, lakini changamoto za elimu, zilimkwamisha.

Kijana Abdul -Azizi akisimulia alikopita shuleni, alikabiliwa na changamoto kukosa mkalimani wa lugha ya alama shuleni na kumsababisha achukue hatua ya ziada apate uelewa, jambo lililompa ugumu masomoni

Anaeleza, namma ugumu huo ulivyo, ni mwalimu anapofundisha bila ya mkalimani, inamuacha nyuma kimawasiliano, tofauti na wanafunzi wengine, hata ikambidi kutafuta wakalimali wa kujitolea kumfafanulia anachozungumza mwalimu.

Kuhusu siri ya mafanikio yake, anadokeza ni juhudi za kusoma, pia msaada wa walimu wake, wazazi na wakalimani, waliojitolea shuleni, hali kadhalika ushirikiano kutoka kwa wanafunzi wenzake shuleni.

“Mwalimu anapomaliza kusomesha darasani huwa sioni tabu kuuliza pale ambapo sijafahamu au huwauliza wanafunzi wezangu na wakinipa ushirikiano mzuri bila ya kuninyanyapaa”anasema.

Sasa anasema malengo yake ya baadae ni kuwa daktari wa binadamu, kwa ajili ya kutoa huduma za matibabu ya afya kwa wananchi hasa watu wenyeu ulemavum akishauri ni vyema Wizara ya Elimu ikaandaa mitihani maalum kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, ili kuwathmini kwa haki zaidi.

Anasema, wasiwasi wake sasa ni masomo ya kidato cha tano, akifafanua: “Kila ukipanda juu zaidi, masomo ndio yanakuwa magumu kutokana na mazingira ya kupata elimu kwa watu wenye ulemavu, bado sio rafiki sana.”

Mwanafunzi huyo anasema awali alifaulu kuingia shule ya vipawa maalum darasa la saba na kubahatika kupelekwa shule maalum, lakini akashindwa kusoma huko, kutokana na changamoto za walimu wanaofundisha lugha ya alama.



Abdul-Aziz Khamis Ali, akiwa katika chumba cha maabara shuleni, alikosoma. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

### WAZAZI WA WANAFUNZI

Mama wa mwanafunzi huyo, Maua Abdallah (53), anasema mwanawe huyo ni wa sita kati ya watoto wake saba, wawili wana shida ya kusikia tangu kuzaliwa na hajajua sababu, licha ya kuhangaikia matibabu katika hospitali mbalimbali.

“Hali yake tumeipokea na tunampa haki zake zote zinazostahiki ikiwamo elimu,” anasema mama huyo, huku baba wa mwanafunzi huyo, Khamis Ali (67), anaelekeza pongezi kwa serikali kupitia Baraza la Watu wenye Ulemavu, kwa msaada wa kuwajali watoto wenye ulemavu na kufuatilia maendeleo yao.

“Dada yake Abdulazizi ambaye nae ni kiziwi, anasoma elimu ya juu Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), lakini ada ya chuo analipiwa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Watu, Wenye Ulemavu maana hali zetu za kiuchumi ni duni sina uwezo wa kumlipia ada,” anasema, akiiomba serikali kuajiri wakalimani kuwawezesha darasani wanafunzi wenye uziwi.

### JUMUIYA WAKALIMANI

Muhammed Wahabi kutoka jumuiya ya wakalimani wa lugha ya alama Zanzibar (JUWALAZA), anasema lugha ya alama alianza kujifunza darasani wakati huo akisoma shule pamoja na wanafunzi viziwi lakini baada ya kuingia kidato cha tatu aliacha kuwasiliana na viziwi kwa sababu hawakufanikiwa kuendelea na masomo.

Anasema baada ya kukutana na mwanafunzi Abdul-Azizi mwaka 2021 wakati akimfundisha masomo yake katika muda wa masomo ya ziada (Tuisheni) ndipo alipomshauri kwenda kusoma lugha ya alama ili kumsaidia katika mawasiliano hasa katika masomo yake.

Wahabu anasema, hakupuuza ushauri wake na ndipo alipoanza

INAENDELEA UK.13

ELIMU NA SABATO KASIKA

NYAYO ZA MEI MOSI NA KUSHUKA ELIMU...

# Wenye fani wafunguka kinachowasibu

KILA mahali nchini kitaifa na kimataifa kuna kilio 'kiwango cha elimu kimeshuka'. Hapo inakumbusha nafasi yake kwa maisha ya kawaida ya watu kuanzia sasa hadi wakati ujao.

Ndiyo maana muasisi wa taifa, Mwalimu Julius Nyerere, tangu akabidhiwe usukani kuongoza nchi, mipango na sera zake hazikuiweka kando. Itakumbukwa ni sekta inayobeba asilimia kubwa ya bajeti ya nchi kufika asilimia 25 katika zama hizo.

Inaporejewa kitaaluma, elimu ambayo Nyerere akaibatiza 'ufunguo wa maisha', ni maarifa, ujuzi na utashi (kama falsafa, itikadi na imani) wa maono ya maisha anayopewa binadamu kuyamudu na kuyasimamia.

Hata haja ya elimu kumfikia binadamu, kunahusika nyenzo kuu tatu ambazo ni: Mwanafunzi anayefunzwa; mtoaji elimu ambaye ni mwalimu; pia msimamizi na mmiliki mkuu wa mfumo wa elimu hiyo, kwa maana ya mahitaji kama miundombinu hitajika, mitaala, huduma za mahitaji yote, ikiwamo ujira kwa mwalimu.

Utatu huo mara zote unatakiwa kila moja utende yake kwa ufanisi, usahihi na tija ya ziada inapobidi, vilevile mapengo yanayoleta kasoro daima yaepukwe kadri inavyowezekana.

Bado elimu ndio inayozalisha kila kitu kinachoendelea duniani, kuanzia uelewa wa msingi, kuzalisha wataalamu, mwendelezo wa utafiti na stadi za kiteknolojia, hali kadhalika ushauri wa kitaalamu.

Pia, ikirejewa utafiti wa kiuchumi unaotafsiri nyenzo za maendeleo ikiwamo fedha za kuhudumia, nguvukazi ya mwanadamu inatajwa kuwa ngazi ya juu, kwa sababu ndio inatenda kikazi, vilevile inasimamia mahitaji yote. Mfano, licha ya kuwapo vyote hospitalini, daktari na watendaji wa kitalaamu wanabaki ni watendaji wanaoendesha shughuli, vilevile wanasimamia vyote.

Mtazamo huo anaporejeshewa mwalimu na watendaji wengine kitaalaamu, pia wasiokuwa wataalam, wanabeba mzigo wa ufanisi, ikiwamo kuendesha mihimili mitatu yote inayohitajika kisekta.

Katika sura ya pili, mwalimu huyo ni binadamu aliyewekeza nafsi yake katika sekta yake, hata akirejeshewa kiajira, anahitaji ya kukidhi mahitaji yake ya kila siku kama binadamu yeyote.

Vilevile ikiazimwa nadharia ya rasilimali watu, hata saikolojia kwa ujumla, binadamu akiwamo mwalimu, ufanisi wake unapatikana anapokidhi mahitaji yake ya kimaslahi, mazingira sahihi kikazi, hata akawawezesha wanafunzi wake kupokea ufanisi wake, kupitia mwongozo wa mitaala, sheria, taaluma na utashi binafsi.




Mwalimu akiwajibika darasani. **PICHA: MTANDAO**

> Ni suala lililoibuliwa tena katika hotuba ya wadau, kwa Rais Dk, Samia Suluhu Hassan, jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi, ambaye naye akawaahidi kuishughulikia.

Je, hicho kinawafikia walimu? Kuna usemi, "hoja kwa vielelezo". Jana katika toleo la Mei Mosi, gazeti hili lilikuwa na simulizi mahsusi ya mwalimu kutoka wilaya ya Tanganyika mkoa wa Katavi, aliyefungiwa mshahara wa miezi kadhaa, kisa na mkasa anadai ni kufuatilia stahiki zake za uhamisho kisheria uliofanywa na mwajiri.

Ni sakata lililochukua zaidi ya mwaka mmoja na mmoja wa wahusika wakuu wa magumu hayo, anatajwa ni ofisa elimu husika, ambaye pia ni mwalimu aliyepewa dhamana kiuongozi kwenye halmashauri, kusimamia sekta ya elimu mahali hapo.

Mwalimu amalalamika amekuwa akihangaika kila mara kwenye kituo kipya cha kazi, akiacha familia nyumbani, kashindwa kuihamisha mizigo yake na kuna wakati analazimika kurejea kwenye kituo cha zamani, hata akaelezwa na wakuu wake kuendelea kufundisha kwa muda.

Pale, akalalamika kila anapofuatilia zaidi stahiki za kuhama, anaishia kusimamishiwa mshahara kwa miezi kadhaa, hata chama cha walimu kikaamua kumsaidia kwa ngazi ya kisheria.

Hapo inarejesha mtazamo kama huo kuendelea hadi sasa kwenye sekta ya elimu, ilhali ngazi ya kitaifa kukisikika mapambano 'kumsaka mchawi' anayeangusha elimu, ulinganifu inatoa tafsiri gani?

### MSTAAFU AFUNGUKA

Philomena Mosha, ni mwalimu mstaafu mkoani Dar es Salaam, anasema maslahi ya walimu ni nyenzo muhimu kwa maendeleo kitaaluma kwa wanafunzi, hapo anashauri ni muhimu kutafakari kwa kina kuhusu mustakabali wa maendeleo ya taaluma, kwa kusimamia nyenzo hiyo yenye mchango mkubwa kuinua elimu.

"Walimu hawapati hata chai shuleni, badala yake wanatoka nayo nyumbani na kiporo cha wali au kama kuna shule kuna wafanyabiashara wadogo, wanatozwa ushuru, halafu pesa inayopatikana, mwalimu mkuu anawanunulia walimu sukari," anasema Mwalimu Philomena.

Anafafanua uzoefu wake, alianza kazi mwaka1985 na kustaafu 2020, hakuwahi kusikia posho ya kufundishia. Haoo anaendelea: "Katika hali hiyo malalamiko ni mengi. Ni vigumu walimu kusimamia vizuri masomo darasani, matokeo ni kushuhudia kiwango cha kufaulu kikishuka siku hadi siku."

Mwalimu huyo anasimulia hali hiyo inayodhoofisha tija ya mto elimu, anasema walimu hukutwa na mahangiko ya kutafuta stahiki zao pasipo mafanikio na wanajikuta wakitumia muda mrefu nje ya madarasa, wakikata tamaa na kutofundisha kwa moyo.

### HALI YA UFAULU

Mwalimu Philomena anasema, hali ya taaluma na viwango vya ufaulu wa wanafunzi si nzuri, akitoa mfano ufaulu wa wanaohitimu darasa la saba na kupata wastani wa daraja A hadi C umeshuka kwa miaka mitatu mfululizo.

Anafafanua matokeo yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) kati ya mwaka 2020, 2021 na 2022, ufaulu ulishuka kutoka asilimia 81.97 hadi asilimia 79.62.

"Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi nao unaendelea kuzorota, kwani unaweza kukuta mwalimu mmoja kwa wanafunzi 65 kwa shule za umma mwaka 2022 ukilinganisha na wanafunzi 62 mwaka 2021. Hizo ni taarifa zilizopo TAMISEMI," anasema.

Anatoa mfano, kuna wakati mwalimu huyo mwenye maslahi duni anafundisha wanafunzi 200 darasani, hali inayoua ari, ingawa ni taaluma ya wito. Kwa mujibu wa viwango vilivyopo, darasa moja linapaswea kuwa na wanafunzi wasozidi 45, akiendelea: " Ni vigumu kufundisha kwa moyo bila maslahi, huku wakiona watumishi wa kada nyingine wana maisha mazuri, wao wakibaki nyuma."

### MBUNGE ALIA NA POSHO

Katika kikao cha bunge hivi karibuni jijini Dodoma, Mbunge wa Kilwa Kusini mkoani Lindi, ambaye pia ni mwalimu mstaafu, Ally Kasinge, akichangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka ujao wa fedha, anataka kuwapo posho ya ufundishaji, kwani kukosekana kwake kunachangia kushuka kiwango cha elimu nchini.

Ni suala lililoibuliwa tena katika hotuba ya wadau, kwa Rais Dk, Samia Suluhu Hassan, jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi, ambaye naye akawaahidi kuishughulikia.

Kwa mujibu wa mbunge Kissenge, kuondolewa posho hiyo ni kikwazo kwa tija darasani na ikirejeshwa, itasaidia msukumo wa ufaulu, kwani kutaleta ufanisi, akikumbusha iliwahi kuuwapo huko awali. Pia, anashauri haja ya kuwapo mpango wa masomo wenye vifaa visaidizi vya kufundishia, ikiwamo midoli kwa wanafunzi wadogo.

# Mwanafunzi asiyesikia awapiku wazima kwenye mtihani, akilenga kuwa daktari

INATOKA UK.11

kujifunza lugha hiyo ya alama, baada ya kuona jitihada zake kutafuta elimu na ufahamu wake ni mzuri kuliko kwa wale wasio na ulemavu.

Anasema alijifunza lugha ya alama kutokana na msukumo wa mwanafunzi Abdul-Azizi na alipoijua lugha hiyo, akamshawishi tena akaombe shuleni anakosoma, ili kuwasaidia wanafunzi viziwi w Shule ya Dk. Magufuli.

"Nashukuru nilipoenda kuomba kujitolea shuleni hapo, niliruhusiwa nikawa nawasaidia wanafunzi viziwi katika masomo yao kwa muda wa miaka mitatu tokea mwaka 2020 hadi 2022 baada ya serikali kupitia wizara ya elimu kusitisha vijana wanaojitolea ambao hawajaajiriwa," anasema.

Anafafanua kuwa, nje ya Shule Abdul-Azizi alianza kumfundisha lugha ya Kiingereza na yupo vizuri katika lugha hiyo ambayo imemuwezesha kufanya vizuri katika mitihani yake.

Pia, anafafanu kwamba, ingawa hayakuwa matarajio yake mwanafunzi wake kupata daraja la pili la ufaulu, akitarajia daraja la kwanza, hata anayatathmini ni matokeo ambayo yamemfiji sana.

Sasa anashauri kiseriali, elimu mjumuisho iboreshwe zaidi ili watu wenye ulemavu kuwekewa miundombinu rafiki katika kupata elimu.


Swafinia Ali Salum, ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Dk. Magufuli ambae anashughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo shule hiyo kwa sasa inawanafunzi saba wenye ulemavu wakiwemo viziwi na waviungo.

Anasema shule hiyo inafuata muongozo wa elimu mjumuisho ambapo wanafunzi wote wenye ulemavu na wasio na ulemavu kuchanganywa darasa moja kwa kupata elimu.

### ALIYEMFUNDISHA SHULE

Mwalimu huyo anamuelezea mwanafunzi wake Abdul-Azizi licha ya kwamba ana ulemavu lakini ni mwanafunzi hodari anayependa kujifunza na hufanya vizuri kuliko wanafunzi wasio na ulemavu, akifafanua shule hiyo hutoa elimu kwa wanafunzi wasio na ulemavu na hakuna tabia ya kuwanyanyapaa, bali wanapewa ushirikiano.

Akizungumzia kuhusu vifaa au visaidizi kwa watu wenye ulemavu, anasema kwa upande wa viziwi, hakuwa na visaidizi vya aina yoyote, ila kwa kwa walemavu wa viungo, shule hiyo ina miundombinu rafiki, ikiwamo katika majengo yke ya ghorofa.



Mwanafunzi Abdul-Aziz Khamis Ali, akiwa darasani katika Shule ya Sekondari Dk. John Magufuli, mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Anasema shuleni hapo kuna changamoto kubwa ya wakalimani kwa wanafunzi viziwi hasa baada ya kuondoka kwa walimu wa kujitolea ambao waliokuwa wakiwasadia wanafunzi viziwi katika lugha ya alama.

"Mimi nawashughulikia wanafunzi wote wenye ulemavu na wasio na ulemavu na mimi nasomesha somo la Kiswahili na historia sasa ninapofundisha huwa natumia sauti na ishara yaani lugha ya alama ili wanafunzi viziwi nao kufaidika ingawa mimi sijasomea lugha ya alama lakini nimejifunza kutoka kwa wanafunzi viziwi"anasema.

Anasema matarajio yake ni kwenda kusomea lugha ya alama ili kuwaondoshea vikwazo katika shule hiyo kwa wanafunzi viziwi kupata elimu.

Aidha anasema amefarajika sana ufaulu wa mwanafunzi wao Kiziwi hivyo wanafunzi wenye ulemavu wakiwekewa mazingira mazuri wanauwezo wa kufaulu vizuri katika masomo yao.

### WIZARA YA ELIMU

Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuna wanafunzi 26,169 walifanya mitihani ya kidato cha nne Zanzibar mwaka jana, kati yao 14 ni wenye ulemavu kutoka shule za serikali za Unguja, akiwemo Abdul-Azizi.

Juma Salum Ali, ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, anasema kabla ya mwaka 2004 kuanza mfumo huo wa elimu mjumuisho, wanafunzi wenye ulemavu walikuwa wanasoma katika mazingira magumu zaidi.

Ali anadems, mfumo umesaidia wanafunzi wengi wenye mahitaji maalum, fursa ya kupata elimu na sasa, kuna wanafunzi 7,314 wenye ulemavu mbalimbali katika shule za serikali, kuanzia ngazi ya maandalizi, msingi na sekondari na wanafanya vizuri katika mitihani, mchangio kmkuu ni msaada wanaopata.

Pia, anataja mkakati wanaotumia katika kupunguza changamoto hiyo, ni kuwafundisha walimu lugha ya alama nai elimu hiyo haishii kwa walimu pekee, hata kwa wanafunzi wasio na uziwi, ili wawasaidie wenzao wahitaji wa msaada.

Katika vifaa visaidizi kwa wanafunzi wenyeulemavu, mkuu wa kitengo hicho, anasema serikali imejitahidi kuwanunulia wanafunzi hao vifaa, hata anakiri havitoshelezi mahitaji, ikiiwamo kwa wenye shida ya kusikia.

"Wizara imenunua vifaa vingi kwa wanafunzi wenye ulemavu kwa Shule za Unguja na Pemba ambapo gharama ya vifaa hivyo ni zaidi ya shilingi milioni 400," anadems, hukia kirejea upande wa pili, kwa sasa wazazi wengi wanahamasika kuwapeleka shule watoto wao wenye ulemavu.

### WADAU WASAIDIZI

Mwenyekiti wa Umoja wa watu wenye Ulemavu Zanzibar, Salma Saadati, anasema elimu kada hiyo kwa sasa inatoa matokeo chanya, ikilinganishwa na nyuma wanafunzi hao walikosa haki.

> Idadi ya viziwi Zanzibar inaongezeka, hivyo ni vyema kuwa na wakalimani ambao watakidhi mahitaji katika kila sekta na si kwa sekta ya elimu pekee.

Anasemas, Wizara ya Elimu, ina jukumu la kuajiri wakalimani, kuwasaidia wanafunzi viziwi kupata elimu na kufaulu mitihani yao vizuri.

Mwadawa Khamis, Mwenyekiti wa Shirikisho la Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA), anasema wanafunzi wenye uziwi, wanahitaji jitihada za ziada kuwapatia elimu na kwenye lugha ya alama, iwe somo la lazima kwa wanafunzi wote.

Anasema, wanafunzi wengi viziwi huvunjika moyo, hata kuwafanya kutoroka shule kutokana na changamoto za kupata elimu, hasa kukosa mawasiliano yao.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, Ussi Khamis Debe, anashauri Baraza la Mitihani Zanzibar, wanapotoa matokeo ya wanafunzi, waweke mahsusi ufaulu wa wenye ulemavu kwenye mitihani hiyo ya taifa.

Anasema hali ilikofika, jamii imeshapata mwamko kuona watu wenye ulemavu wana haki ya kupata elimu, ingawa kiwango chao cha ufaulu bado kidogo, kwani kuna changamoto nyingi kwao katika kujifunza.

"Idadi ya viziwi Zanzibar inaongezeka, hivyo ni vyema kuwa na wakalimani ambao watakidhi mahitaji katika kila sekta na si kwa sekta ya elimu pekee"anasema.

Anasema tayari Sheria mpya Namba Nane ya Mwaka 2022 ya Watu Wenye Ulemavu, imeshapitishwa na kutiwa saini na Rais, ikiopatia meno ya kusimamia majengo yote ya umma kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu, akishauri kila mzazi anapaswa kusimamia masklahi ya watoto wao wenye ulemavu.

### WAZIRI WA ELIMU

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Leila Muhammed Mussa, anasema wizara hiyo inaendelea kuboresha sekta ya elimu, ili watoto wote kupata elimu bora, ikitarajia kuajiri walimu mahsusi wa lugha ya alama shuleni, pia inamalizia ujenzi wa shule mbili za elimu mjumuisho, za Jendele, Unguja na Pujini, Pemba.

"Shule hizi zitakuwa na vifaa vya kisasa kwa watu wenye ulemavu katika kupata elimu lakini pia shule hizo zitakuwa na bweni ili wanafunzi wenye mahitaji maalum kupata mda wa ziada wa kufundishwa masomo yao," alisema Waziri huyo.

TEKNOLOJIA

NA HALFANI CHUSI

BAADA KASORO ZISIZOISHA KILA SIKU...

# Watumia pikipiki waingiziwa darasa la kiufundi kufikia ufanisi kutumia

UNAPOTAJA pikipiki leo hii, imekuwa sehemu ya maisha ya umma. Ni chimbuko la usafiri 'hapa na pale', imeajiri wengi kuanzia wanaoendesha, mafundi wake wanaoziuza hadi mnyororo mrefu wa kuiagiza ng'ambo ya mbali.

Hata hivyo, kukosekana elimu sahihi ya kutunza chombo hicho, kunatajwa kuwa sehemu ya ustawi wake. Moja ya sababu inatajwa kwa vyombo vingi vya moto kutodumu kwa muda mrefu au kusababisha ajali na kutokugunduliwa tatizo mapema.

Sasa kuna hatua inapigwa ya kuwapo elimu mahsusi, kumsaidia yule aliyekosa stahiki hiyo, pikipiki tajwa haidumu muda mrefu, kwa kukosekana elimu ambayo wengi wameikosa, lawama zikiwarejea wanaotengeneza.

Moja ya kampuni husika inayotengeneza pikipiki imeamua kuchukua hatua, Nipashe ikiwa shuhuda wa hatua hiyo, kutokana na kukosekana elimu tajwa. Kupata undani, hapo ndipo Nipashe ikalazimika kufunga safari mpaka makao makuu ya kampuni inayohusika na biashara za kampuni ya TVS, ikataka ufafanuzi.

Fundi wa pikipiki kutoka kwenye kampuni hiyo, Yusuph Bakar anaelezea:"Ikiwa unataka kutumia pikipiki kwa muda mrefu, unahitaji kujua jinsi ya kuitunza. Hii itakupunguzia shida na safari za mara kwa mara kwenda gereji, pia kuihudumia mtumiaji mwenyewe bila kwenda kwa fundi. Utahitaji tu kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na mabadiliko ya kiufundi."

Anaanzisha darasa, katika kipengele cha ufuatiliaji injini. Hapo anafafanua kwamba, injini ndio moyo wa pikipiki na ndiko kwenye msingi na jinsi mashine ya chombo inavyofanya kazi kuendesha pikipiki na injini iliyoharibiwa inatia ugumu wa safari. Hapo anasema ndiko kuna sababu mtu anapaswa kuangalia kila wakati hali ya injini ya pikipiki yake.



Fundi pikipiki wa kampuni ya TVS (mwenye tisheti ya bluu), Yusuph Bakari, akitoa elimu ya utunzaji chombo hicho kwa baadhi ya madereva, ili kuwawezesha kutunza vyombo vyao. **PICHA: HALFANI CHUSI**

Pili, anataja kwenye kilainishi (oil) kwamba, nilazima ibadilishwe kulingana na maagizo ya muuzaji pikipiki au kufuata maagizo yaliyoko kwenye kitabu cha matengenezo ya pikipiki.

Anasema, huduma hiyo inapaswa kufanywa kila baada ya wiki mbili, ikiwa mtumiaji ataenda na kilainishi pendekezwa kama alivyoshauriwa na muuzaji chombo.

Vilevile hoja hiyo inaendana na udhibiti wa vichujio; hapo kunatajwa ni kuangalia chujio la hewa na chujio la mafuta. Hapo fundi Bakari anafafanua jukumu la chujio la hewa ni kuhakikisha uhamishaji sahihi wa hewa kwa injini na lazima itunzwe vizuri, ili kuepuka matumizi mengi ya petroli. Anasema, hiyo itaruhusu injini ya pikipiki kufanya kazi vyema, ikiwa na nguvu zaidi.

Ili kushughulikia chujio la hewa, anasema inapaswa kusafishwa mara moja kwa wiki kama inavyoshauriwa na mtengenezaji au msambazaji, pia inapaswa kubadilishwa baada ya safari kilomita 12,000.

Kwa upande wa chujio la mafuta, anasema inasaidia kuondoa uchafu wote unaotokana na matumizi ya kiminimika hicho na kazima ikaguliwe na kusafishwa mara moja kila wiki, ili kupatikana ufanisi bora wa chombo.

Pia, anataja ili kukifanya chombo chako kidumu, mtumiaji anapaswa kujenga utamaduni wa kukagua na kubadili chombo plagi, kuhakikisha uchomaji moto kwenye chombo unakuwa wa uhakika,

Hili ni jambo linalopaswa kuzingatiwa sana Maisha ya plag ya pikipiki ya TVS ni kimomita 12,000, hivyo mteja anapaswa kubadili baada ya kufikia muda huo. Pamoja na kutumia vipuri halisi kutoka kwa wasambazaji walioidhinishwa.

Anashauri mwendesha pikipiki anapswa kuangalia kiwango cha betri kila mara, ili pikipiki husika ifanye kazi kwa ufanusi, wastani ya miaka miwili. Hapo mtumiaji anapaswa kukagua kiasi cha maji na kiwango cha chaji, pia anashauriwa kujaza maji kweneye betri yanapokuwa yamepungua

Ligine linatajwa ni ukaguzi na kurekebisha 'gepu' la kucheza kwa mnyororo, kusafishwe na kulainishwa mara moja ndani ya wiki mbili, pia mnyororo unapolegea, unaongeza ulaji mafuta kwenye chombo, vilevile mnyororo huo unapokazwa sana, nao unaleta athari kwenye vipuri vilivyofungwa kwenye pikipiki husika.

Fundi Bakari anaeleza kwamba, penye mfumo wa taa ya pikipiki, nao unatajwa kuhitaji uangalifu akiwa na angalizo kwa dreva aliyezoa kutumia taa usiku, kamwe mtu asiendeshe barabarani na taa zilizo na kasoro, bali akague mfumo wa taa ya pikipiki kabla ya kuiendesha.

Anasema, ni hali inayomruhusu mwendeshaji kuona vizuri, kwa taa zote zinafanya kazi kwa usahihi anapogundua balbu zake haifanyi kazi au inaonekana kwa dhaifu, daima ashughulikie kuibadilisha.

**USAFIRI NA BREKI**

Rai ya fundi huyo ni kuwapo utaratibu bora wa kukakgua breki, ilikumuweka dereva na chombo chake salama hivyo wakati wa uendeshaji inapaswa kuwa katika hali nzuri, haijalishi unasonga haraka vipi.

"Tunapendekeza kufuata maagizo ya mtengenezaji ya kuangalia breki, lakini kwa ujumla, breki zake zinahitajika kuchunguzwa kila baada ya kilomita 1,000 au kila baada ya wiki mbili. Hiyo inakufanya kujua kama pedi zimechoka au la," anasema Fundi Bakari.

Anaendelea" "Kwa kuongeza, kuna mambo kadhaa yanayoweza kuonyesha kuwa ni wakati wa kubadilisha breki. Kwa mfano, ikiwa unasikia kelele ya 'rimu' wakati wa kushika breki, pamoja na kuchelewa kusimama unapofunga breki."

Pia, anataja uamkini kuisafisha pikpiki nzima, baada ya kukagua vifaa vyote vya pikipiki, ili kuifanya nadhifu. Bakari anafafanua faida nyinginezo, ambazo ni kutoa mchanga kwneye sehemu mbalimbali za pikipiki, kukiwapo tahadhari ya kuepuka kutumia maji yenye chumvi.

## WANENAVYO MALENGA

### MAMA MKWE KIVURUGE

Mama mkwe kivuruge, huyo ni hasara kubwa,
Ni sawa na kula zege, na wala siyo ubwabwa,
Nyumba aleta matege, na hata vurugu kubwa,
Mama mkwe mkorofi, ni bora kumuepuka.

Mama mkwe mkorofi, ni bora kumuepuka,
Utasema mbona hafi, uweze kupumzika,
Sawa na bidhaa ghafi, haifai kutumika,
Akija ni tumbo joto, amani inatoweka.

Akija ni tumbo joto, amani inatoweka,
Jinsi anawasha moto, yake mwanae ashika,
Linatawala fukuto, hadi atapoondoka,
Amri nyumbani kwake, ndizo zinahamishika.

Amri nyumbani kwake, ndizo zinahamishika.
Ndoa yenu yawa yake, afanya analotaka,
Yadumu mipango yake, yenu chini anaweka,
Kuoa na kuolewa, kunakuwa kuteseka.

Kuoa na kuolewa, kunakuwa kuteseka,
Yake ndiyo yaenziwa, hata kutekelezeka,
Ya mwenza yanafukiwa, hata ya kueleweka,
Kuja kwake wajutia, badala kushereheka.

Kuja kwake wajutia, badala kushereheka,
Aja unafikiria, ni lini ataondoka,
Ili yako familia, ipate stareheka,
Mama mkwe huyo zigo, gumu sana kubebeka.

Mama mkwe huyo zigo, gumu sana kubebeka,
Tena huyo ni kigogo, kwa mwanaye apendeka,
Lazima uweke logo, ya kwake kuvumilika,
Akisema hakutaki, ndoa yaweza vunjika.

Akisema hakutaki, ndoa yaweza vunjika,
Yake kwa mwanaye tiki, ndiyo yanaaminika,
Tamani akulaiki, usibaki takataka,
Mama ni mvunja ndoa, pia aweza simika.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Serikali yaombwa kutenga bajeti shule za sekondari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kutenga bajeti kwa ajili ya wanafunzi wa shule za sekondari wenye uwezo wa kubuni mifumo ya kuondoa kero za jamii ili kuwasaidia kukuza vipaji vyao na kuingia kwenye soko la ushindani.

Mkuu wa taaluma wa Shule ya Sekondari ya St. Peter Claver, Jeanett Dmello, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipopokea tuzo ya ushindi wa pili ya wanafunzi wa shule hiyo waliobuni mfumo wa upigaji kura kwa njia ya kieletroniki pamoja na mashine ya kufyonza vumbi.

Alisema ili kukuza vipaji vya wanafunzi ambavyo wanavionyesha kwenye wiki za ubunifu, serikali inapaswa kuendeleza ili ujuzi wa vijana wadogo usipotee kadri wanavyokua.

Dmello alisema shule hiyo imejipanga kumtengeneza mwanafunzi katika nyanja tofauti ili awe bora darasani, lakini pia awe bora kwenye ujuzi mbalimbali kwa ajili ya faida yake ya baadaye.

"Tumekuwa tukiwafundisha darasani wanafunzi wetu, lakini kwenye kitengo cha sayansi na vitengo vingine shuleni hapo wanafunzi wamekuwa wakibuni mawazo yao na walimu kuwapatia nini cha kufanya ili bunifu zao ziboreshwe na kuingia katika mashindano au maonyesho ya ubunifu," alisema D'mello.

Naye, Mkuu wa shule hiyo, Father Buberwa Karongo, alisema shule hiyo inatoa nafasi kwa wanafunzi ya kuhudhuria makongamano mbalimbali ya ubunifu lengo ni kutaka kubadilishana mawazo na watu ili kuzidi kuongeza ujuzi walionao.

Alisema katika ubunifu wa mashine ya kufutia vumbi walioibuni inatumia umeme na betri.

Akizungumzia ubunifu wa mashine hiyo, mwanafunzi wa kidato cha nne wa shule hiyo, Patricia Mhilu, alisema mashine hiyo ni nzuri kwa ajili ya kufutia vumbi na inatumika mahali popote na inasaidia kuwapunguzia adha wale ambao wanaumwa mgongo na hawawezi kuinama kupiga deki.

# Mtandao wa kijamii wenye usalama maongezi wabuniwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (eGA), imebuni mifumo nane ya mawasiliano ikiwamo mtandao wa kijamii 'Oxygen' wenye usalama wa hali ya juu kwenye maongezi ya sauti na ujumbe mfupi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kilele cha maadhimisho ya wiki ya ubunifu kitaifa jijini hapa juzi, Ofisa TEHAMA wa mamlaka hiyo,

Tumaini Masinsi, alisema mtandao huo wa kijamii uliundwa kwa lengo la kufanya mawasiliano kwa ujumbe mfupi, sauti pamoja na kutumiana picha.

"Mtandao huu unapatikana kwa njia ya tovuti na programu ya simu kwa android na IOS," alisema.

Aidha, alisema wamebuni mfumo wa kuratibu shughuli za kimawasiliano kwa kupiga simu kwa taasisi mbalimbali za umma.

"Mfumo huu ni mahususi kwa ajili kuongeza ufanisi wakuhudumia wananchi wenye malalamiko, maulizo mapendekezo, na pongezi," alisema.

Pia alisema mfumo mwingine unaotumia teknolojia ya akili bandia kusaidia mamlaka hiyo kujibu maswali ya mara kwa mara kuhusiana na utendaji kazi wa mamlaka.

"Tumebuni mfumo wa kutuma, kupokea na kufuatilia malalamiko, mapendekezo, maulizo na pongezi kwenda kwa taasisi mbalimbali za umma," alisema.

Masinsi alisema kuna mfumo wa kuratibu vikao vya bodi na kamati zake, menejimenti na kamati zake pamoja na madiwani.

"Mfumo huu umekua suluhu kubwa kupunguza gharama za utendaji kazi kwenye eneo hili la vikao," alisema.

Naye, Ofisa TEHAMA wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa umma na Utawala Bora, Osea laizer alisema ubunifu umelenga kusaidia makundi mbalimbali wakiwamo watumishi wa umma.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (kulia), akisalimiana na Mbunge wa Liwale mkoani Lindi, Zuberi Kuchauka, nje ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zimamoto yataka michoro majengo shule kukabiliana majanga ya moto

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limeshauri uongozi wa shule mpya zinazojengwa kuwasilisha michoro ya majengo yake kwenye jeshi hilo ili lishauri mifumo na miundombinu ya kukabiliana na majanga ya moto shuleni.

Kamanda wa Jeshi hilo mkoani Singida, Mrakibu Devotha Bigawa, aliyasema hayo juzi mjini hapa alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa elimu.

Alisema suala la kukabiliana na majanga ya moto sio la Zimamoto pekee bali linahitaji ushirikiano wa watu wote kuhakikisha miundombinu ya umeme inakuwa salama kwenye majengo. Bigawa alisema sheria ya majengo ya mwaka 2015 kanuni ya 248 na marekebisho yaliyofanyika 2022 inaelekeza kabla mamlaka nyingine hazijapitisha kuanza kwa ujenzi wa jengo fulani inatakiwa mchoro wa jengo husika upelekwe Zimamoto ili kushauri namna ya kuweka miundombinu hiyo.

Bigawa aliwahimiza walimu wajenga utamaduni wa kufanya ukaguzi miundombinu ya umeme kwenye shule zao kwa kuwa licha ya baadhi ya shule kutoruhusu wanafunzi kuwa simu wanapokuwa shule, lakini wanafunzi wamekuwa wakitumia ujanja wa kuzichaji kwenye dali na kukata umeme hali ambayo ni hatari.

Aidha, aliwataka walimu kushirikiana na klabu za moto ambazo zimeanzishwa kwenye shule kwa kuwa wapo wanafunzi wamepewa mafundisho ya namna ya kuzima moto katika hatua ya awali kabla Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halijafika katika eneo la tukio.



**HABARI MBEYA**

# Jengo CCM laanza kujengwa baada ya kuwa na mvutano

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

UJENZI wa Ofisi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya uliokuwa umekwama kwa muda wa miaka mitatu kutokana na mvutano wa kisiasa ya baadhi ya viongozi, umeanza.

Jengo hilo lililopo Kyela mjini lilianza kujengwa mwaka 2020, lakini likasimama baada ya kufika kwenye mtambaa wa panya kutokana na sintofahamu ambayo mpaka sasa bado haijawekwa wazi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama hicho Taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alipokuwa kwenye ziara ya kujitambulisha wilayani humo aliagiza ujenzi huo uendelee na kuahidi kutoa mbao kwa ajili ya kuanza kuezeka.

Mwishoni mwa wiki Mwaselela alikabidhi zaidi ya mbao 1,200 na kuagiza waanze kupiga kenchi na kuwaagiza viongozi wa chama wilaya kuezeka haraka.

Alisema endapo viongozi wa chama hicho wilaya watashindwa kukamilisha ujenzi wa jengo hilo, ofisi zilizopo zitabomolewa ili wasiwe na eneo la kukaa na kufanya kazi.

"Hizi mbao nimezinunua kwa Sh. milioni 3.55 kwahiyo hiki ni kipimo tosha kwenu viongozi hasa Katibu, hizi fedha zilikuwa zinatosha kujenga ukuta kwenye eneo lingine lakini nimewapatia ninyi, nataka wiki ijayo muanze kupigilia makenchi," alisema Mwaselela.

Katibu wa CCM Wilaya ya Kyela, Amos Kusakula, alimshukuru Mwaselela kwa mchango huo na kuahidi watakamilisha jengo hilo haraka ili lianze kuwahudumia wananchi wa wilaya hiyo.

Alisema jengo wanalotumia kwa sasa lina hadhi ndogo ambayo haiendani na ukubwa wa chama hicho tawala na watafanya kila linalowezekana wakamilishe.

Alisema kabla ya kuanza kuezeka wamepandisha jengo hilo kutokana na ushauri walioupata kutoka kwa wataalamu ili liwe na hadhi zaidi.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Wilaya ya Kyela, Emmanuel Mwamlinge, alisema migogoro isiyokuwa na msingi wowote imekuwa ikikitesa chama hicho katika wilaya hiyo kwa muda mrefu.

Alisema kwa sasa migogoro hiyo imeanza kupungua baada ya viongozi wa chama mkoa kuingilia kati na kuanza kuwasaidia kukamilisha mradi huo ambao ni muhimu kwa ustawi wa chama.




Mkurugenzi wa Kitengo cha Wateja Wakubwa wa Benki ya NBC, James Meitaron (kulia ) akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Benno Malisa ( wa Pili kulia) pamoja na Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru (Kushoto) na Mkurugenzi wa Bodi ya NBC, Dk Kassim Hussein wakati wa uzinduzi wa NBC Connect , jukwaa la kidigitali la kisasa linalotoa huduma za benki kwa urahisi na salama, wakati wowote na mahali popote kwa kutumia simu ya mtandao (internet). Hafla hiyo ya uzinduzi ilifanyika jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yazindua huduma kibunifu za kidijitali

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BENKI ya Taifa ya Biashara ya (NBC) imezindua huduma ya NBC Connect, ikiwa ni ingizo jipya la huduma za kibunifu za kidijitali katika mkoa wa Mbeya.

Mkurugenzi wa wateja wakubwa wa benki hiyo, James Metairon, amesema huduma hiyo ya kisasa ya kidigitali inalenga kuwezesha huduma mbalimbali salama za kibenki na ambazo zinaweza kufanyika sehemu yoyote, muda wowote kwa kutumia simu ya mkononi na vifaa vingine vinavyotumia intaneti.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa huduma hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijiji hapa, Metairon alibainisha kuwa kupitia NBC Connect, wateja wa mkoa huo na maeneo ya jirani watapata fursa ya kuwa na uwezo wa kufanya miamala yao ya kifedha kwa urahisi zaidi na kupata uzoefu mpya katika kupata huduma za kibenki.

"Huduma hii itawapa wateja wetu uwezo wa kufanya aina zote za malipo ikiwa ni pamoja na malipo ya ndani na nje ya nchi, malipo ya serikali pamoja na malipo kwa mitandao mbali mbali ya simu za mkononi kwa kutumia simu kompyuta, au simu zao za mkononi. Wateja pia watapata mwenendo wa miamala waliyofanya popote pale walipo pasipo kulazimika kwenda benki," alisema.

Alisema NBC Connect imetengenezwa kwa teknolojia ya kisasa na yenye usalama wa hali ya juu ambayo imezingatia na kutoa kipaumbele kwenye usiri wa taarifa za mteja. Ubunifu wa huduma hiyo kuhakikisha taarifa za kifedha za wateja zinalindwa wakati wote.

"Tunafuraha kutambulisha NBC Connect kwa wakazi wa Mbeya na maeneo ya jirani. Mfumo huu wa kibenki wa kidijitali ni uthibitisho wa dhamira ya kuwapatia wateja wetu huduma bora za kibenki ambazo ni rahisi, salama, na zinazofaa na kukidhi mahitaji ya wateja. NBC Connect itawawezesha wateja wetu kufanya huduma zakibenki popote pale, wakati wowote, na kufurahia huduma hizo bila matatizo," alisema.

Alisema pamoja na huduma rahisi na za kisasa, ujio wa huduma hiyo unatajwa kuwa utatoa usaidizi wa binafsi kwa wateja kupitia vituo vyao vya huduma kwa wateja ambapo kupitia mameneja katika vituo hivyo watawasaidia wateja kulingana na mahitaji yao na pia kutoa mwongozo wa jinsi ya kutumia jukwaa hilo kwa ufanisi.

Alisema ili kusherehekea uzinduzi wahuduma hiyo jijini Mbeya, Benki hiyo ilitumia uzinduzi huo kutoa maelezo ya kina juu ya huduma hiyo kwa wateja waliokuwa tayari kujiunga na huduma hiyo ili kuwapa uelewa mpana wa namna ya kuitumia na kufurahia huduma hiyo.

Akiwa katika uzinduzi huo Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Benno Malisa, aliishukuru kwa ubunifu wao mzuri na kuwahimiza wateja kutumia mfumo huo mpya wa kibenki ili kurahisisha shughuli zao za kila siku.

"Uzinduzi wa NBC Connect jijini Mbeya unawakilisha mpango mkakati wa upanuzi wa benki ya NBC ili kuwafikia wananchi wengi zaidi na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi," alisema.

## Rungwe yapata fedha kukamilisha ujenzi madarasa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, imepokea Sh. milioni 970 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika baadhi ya shule za msingi ndani ya wilaya hiyo ili kupunguza matatizo yanayowakabili wanafunzi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, aliyasema hayo alipowasilisha taarifa ya miradi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Mwankuga alisema fedha hizo tayari wameshazipokea na wanatarajia kuanza utekelezaji wa miradi hiyo ili waikamilishe mapema na wanafunzi waanze kuitumia.

"Fedha hizi hazikuwamo kwenye bajeti yetu isipokuwa mheshimiwa rais ametuletea kwa ajili ya kutuunga mkono kwa kazi nzuri tuliyoifanya ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na tayari tumeshazipokea zipo kwenye akaunti," alisema Mwankuga.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, CPA Edward Malima, aliwataka vongozi wa halmashauri kusimamia vizuri vyanzo vya mapato na fedha za miradi ya maendeleo wanazopokea kutoka serikali kuu.

Aliwataka wafenya kazi kwa kuzingatia sheria ikiwamo vikao vya kisheria kama kamati za mipango na fedha, ukaguzi wa miradi pamoja na taratibu zingine za kisheria.

"Lakini pia vikao vya kupokea na kujadili ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), hakikisheni mnakamilisha kabla ya Mei 27, mwaka huu," alisema Malima.

Akiwasilisha salam za serikali kwenye kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu, aliwataka madiwani kushirikiana na wadau wengine kusimamia maadili kwa watoto ili kuepuka vitendo visivyoendana na utamaduni wa Kiafrika.

Aliwataka kutoa taarifa endapo watabaini kuwa kuna makundi ya aina yoyote yanayotoa elimu kwa watoto ama makundi mengine, lakini elimu hiyo haiendani na maadili ili hatua zichukuliwe mapema kabla madhara hayajatokea.

Katika ripoti ya CAG Halmashauri ya Rungwe imepata hati safi na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Renatus Mchau, alisema ushirikiano baina ya wataalamu, madiwani na watumishi wengine wa wilaya hiyo ndiyo waliosaidia kupatikana kwa mafanikio hayo.

# SMZ, SJMT kuweka mazingira bora kwenye sekta ya habari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimesema kuwa zitaendelea kuweka mazingira bora ya kisera na kisheria ili kuviwezesha vyombo vya habari na wanahabari kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, alisema hayo jana wakati akifungua kongamano la maadhimisho ya miaka 30 ya siku ya uhuru wa habari duniani kitaifa lilofanyika mjini hapa.

Alisema hatua hiyo inalenga kujenga uwezo wa vyombo vya habari kufuatilia na kuibua utekekezaji wa mipango, mikakati na miradi ya kitaifa na kimataifa kuwasaidia wananchi kupata maendeleo.

"Serikali zote mbili zinatekeleza miradi ya maendeleo inayowalenga wananchi hivyo waandishi wa habari vinapaswa kufuatilia na kuibua changamoto za utekelezaji wa miradi hiyo ili kuongeza ufanisi," alisema Waziri Tabia.

Akizungumzia sheria mpya ya habari Zanzibar, alisema mchakato wa kupata sheria hiyo umekamilika kwa asilimia 80 na ambayo alisema itakuwa sheria bora itakayorahisisha utendaji kazi wa waandishi wa habari.

"Inakuja sheria moja nzuri sana ambayo itakua rafiki kwa waandishi wa habari na wala msiwe na mashaka kwa hili," alisema Waziri Tabia.

katika hatua nyingine, Tabia alieleza umuhimu wa wanahabari kuendelea kuhamasisha jamii kudumisha amani, utulivu na kutoa habari sahihi zitakazochochea kasi ya maendeleo ya jamii.

Aliwapongeza waandishi wa habari kwa kuendelea kufanya kazi kwa umma na kuimarisha sekta ya habari kupitia maadhimisho hayo.

Alisema wananchi wana uhitaji mkubwa wa kupata taarifa sahihi na ukweli kuhusu hatua za maendeleo za miradi iliyofanywa na serikali chini ya uongozi wa Dk. Samia.

Aidha, Waziri Tabia, alisema dunia hivi sasa inakabiliwa na changamoto kubwa ya uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi na chanzo cha changaamoto hizo yanatokana na binadamu.

Akizungumza katika kongamano hilo Mbunge wa Viti maalum kutoka asasi za kiraia, Neema Lugakingila, alisema vyombo vya habari visipelekeshwe na kasi ya mitandao ya kijamii na baadala yake wafanye habari za uchunguzi ili wananchi wapate taarifa sahihi na zenye manufaa kwa mustakbali wa maisha yao.

Fursa za waandishi wa habari bado hazijafikiwa hasa waliopo maeneo ya pembezoni hivyo ni vyema zikawafikia wa pande zote.

Alisema wanahabari wanatakiwa kujengewa uelewa katika mfumo wa kidigitali ili kwenda na wakati.

Mkurugenzi Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Greyson Msigwa, alisema Tanzania Bara kwa sasa wamefanikiwa kupunguza ugumu wa waandishi wa habari kupata taarifa kutoka kwa viongozi wa taasisi za serikali na kwa sasa pia wametengeneza mkakati wa mawasiliano kitaifa ili kuondoa pia ugumu wa mawasiliano kati ya vyombo vya habari na taasisi za serikali.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Prof. Joyce Ndalichako akikabidhi tuzo ya OSHA mshindi wa jumla wa maonesho ya OSHA Mkufunzi wa Usalama mahali pa kazi wa Barrick Bulyanhulu, Azaely Kitenge,kwa niaba ya kampuni ,katika hafla ya kukabidhi zawadi wa washindi iliyofanyika mjini Morogoro mwishoni mwa wiki (katikati) ni Mwenyekiti wa Bodi ya OSHA, Dk. Adelhelm Meru.Mgodi wa Barrick Bulyanhulu umeibuka mshindi wa kwanza wa jumla katika maonesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaimarisha miundombinu sekta kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema serikali inaimarisha miundombinu katika sekta ya kilimo kwa kujenga mindombinu ya umwagiliaji ikiwamo visima katika mabonde ya wakulima ili kukifanya cha kisasa chenye kuleta tija kwa wakulima na taifa.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa mradi wa umwagiliaji katika bonde la mpunga la kibokwa mkoani humo na Wizara ya Kilimo baada kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, alisema kilimo ni sekta inayotegemewa nchini, licha ya changamoto zinazowakabili wakulima ikiwamo kuingiziwa mifugo, kuchimbwa mchanga pembezoni mwa miundombinu ya umwagiliaji jambo linalosababisha athari katika miundombinu hiyo.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Seif Shaaban Mwinyi, alisema bonde hilo kwa sasa litakabidhiwa rasmi kwa wakulima kutokana na kukidhi mahitaji yote yanayo hitajika katika kilimo cha mpunga wa umwagiliaji kwa kuwa na miundombinu imara na visima vya kutosha vya usambazaji maji.

Naye kiongozi mshauri elekezi wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji kutoka kampuni ya KRC, kutoka nchini Korea, Jang Jeongryeol, alisema wakulima waanze kulima kilimo cha kisasa ili kuzalisha mpunga kwa mwingi.

"Naamini kwamba mradi huu wa umwagiliaji utazalisha zaidi ya mavuno ya mara mbili ukilinganisha na kilimo cha zamani," alisema.

Wakulima wa umwagiliaji bonde la Kibokwa, walisema wameridhishwa na hatua za serikali kwa kuwajali wakulima na sasa wako tayari kwa ajili ya kuanza shughuli za kilimo ili kuleta mageuzi katika sekta hiyo.

## Vyombo vya bahari kupigwa 'stop' kumwaga mafuta baharini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar, imesema itazuia tabia ya baadhi ya wamiliki wa vyombo vya baharini kumwaga mafuta baharini ili kulinda mazingira na viumbe vyake.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, alisema hayo wakati akifungua mkutano wa mashauriano na wadau wa maendeleo ya Kilimo.

Alisema Zanzibar inajenga Bandari ya mafuta Mangapwani ambayo itakuwa na matumizi makubwa ya mafuta na serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo watadhibiti yasiingie baharini kwa kulinda viumbe vya baharini.

Alisema kipaumbele cha kwanza ni kuona viumbe vipo salama katika bahari na kwamba suala la ulinzi wa bahari linahitaji ushirikiano wa pamoja na kudhibiti vitendo hivyo ambavyo vinaongezeka kwa kasi baharini.

"Mafuta yanayozagaa baharini yanaweza kuuwa viumbe na kuharibu mikoko inayotoa hewa safi ya carbon dioxide hivyo tuna kila sasabu ya kulinda baharini," alisema.

Alisema malengo ya serikali yanakwenda sambamba na utekelezaji wa malengo ya dunia ikiwamo kuondoa umasikini, njaa na maradhi ushirikiano na wadau wa maendeleo ya kitaifa yataleta maendeleo kwa serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Aboud Suleiman Jumbe, alisema malengo ya Serikali ya Zanzibar kufikia shabaha zote za mpango wa maendeleo ya taifa ZADEP hasa katika maeneo ya utalii, usafiri wa baharini, uvuvi endelevu, mazao ya bahari na nishati mbadala na mafuta na gesi asilia.

Alisema kuwapo kwa wadau wa maendeleo kumeongeza uwezo wa serikali kufanya utafiti muhimu wa maliasili za bahari na kupata taarifa za utekelezaji wa sera za uchumi wa buluu.

Ofisa kutoka Shirika la Kitaifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Jacqueline Morc Hongu, alisema lengo la kukutana na wadau wa maendeleo ni kufahamu changamoto inayojitokeza kuendesha miradi ya maendeleo ya Wizara ya Uchumi wa Buluu.

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, alisema hayo wakati akifungua mkutano wa mashauriano na wadau wa maendeleo ya Kilimo.**

# HABARI PICHA




Wafanyakazi wa Wizara ya Ujenzi wakipita na bango lao katika maadhimisho ya Mei Mosi . **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia katika Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, katika viwanja vya Nungwi, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: IKULU**



Baadhi ya Mawaziri wa SMZ wakishangilia wakati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani) akihutubia. **PICHA: IKULU**



Mwenyekiti wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT), Wilaya ya Muheza, Mashauri Kanyama aliyenyanyua mkono juu akizungumza neno la mshikamano kwa walimu mahali pa kazi jana katika viwanja vya Bomani, Muheza kabla ya kuelekea Tanga mjini katika maadhimisho ya Sherehe ya Siku ya wafanyakazi. Kulia ni Katibu wa CWT wilaya hiyo, Selemani Mashaka. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Wafanyakazi wa PSSSF wakiwa katika Maandamano ya Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, wakipita mbele ya mgeni rasmi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk.Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: IKULU**

## HABARI KITAIFA

# Maisha feki ya wazazi chanzo watoto kufeli

**Na Mary Geofrey**

MAISHA feki ya wazazi kwa watoto wao yametajwa kuwa chanzo cha mmomonyoko wa maadili na kufeli kwa wanafunzi wengi katika mitihani ya taifa.

Jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Shule Huria ya Skillful Ukonga, Diodorus Tabaro, alitoa kauli hiyo wakati wa mahafali ya 15 ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita waliosoma kwa mwaka mmoja na miezi mitatu.

"Wazazi watumie muda mwingi kuwaonyesha au kuongelea uhalisia wa maisha yenu kwa sababu vijana wengi ambao hawajafanikiwa katika masomo ukiwafuatilia kwa makini unabaini kwa namna moja au nyingine malezi yao yalikuwa feki, sababu mojawapo ni kulelewa na mzazi mmoja pasipo kuzingatia maadili," alisema Tabaro.

Aliwataka wazazi waishi maisha halisi na watoto wao ili wajue wana wajibu wa kuitafuta kesho yao kupitia masomo badala ya kukaa wakitegemea wazazi wao watawasaidia na kuendelea kufanya mambo yasiyofaa ndani ya jamii.

Tabaro aliwataka vijana wanaonza mtihani wa kidato cha sita nchini leo, kuzingatia waliyofundishwa na kutulia wakati wa kujibu maswali ili wafanye vyema.

Alisema shule hiyo inachukua wanafunzi waliofeli masomo ya kidato cha nne, kidato cha sita na ambao hawajapata elimu ya sekondari ambao wanasoma elimu ya sekondari kwa miaka miwili.

Alitaja sifa za kufanya vizuri kwa kundi hilo la vijana ambao wanaonekana wameshindwa kufanya vizuri kwenye masomo ni kuwashirikisha elimu ya dini ili kuwa na hofu ya Mungu, kuwapa ushauri, malezi bora ya maisha na ushauri na kubadili tabia.

"Sisi shule yetu tunaona tabia na malezi vinaenda sambamba. Kila kikoma kikimwacha mwenzake hawatoweza kufanya vizuri, hivyo jambo la kwanza tukichukua wanafunzi waliofeli masomo tunawabadili kwanza tabia ndio sababu wanafanya vizuri," alisema Tabaro.

Mhitimu wa Kidato cha Sita, Anold Mwangile, aliishukuru shule hiyo kwa kutoa malezi bora na kumfanya azingatie masomo kwa kuamini kuwa atafanya vyema katika mitihani yake.

Mwanafunzi Ritha Mahunda alitoa ahadi ya kufanya vizuri katika masomo yake baada ya kujiandaa vyema katika mitihani hiyo.

## Vodacom waja na kampeni kwa wanafunzi vyuo vikuu

**Na Halfan Chusi**

KATIKA kuongeza matumizi ya simu za mkononi nchini, kampuni ya teknolojia na mawasiliano ya Vodacom Tanzania na Infinix, imezindua toleo jipya la simu aina ya Infinix HOT 30 ikiambatana na kampeni maalum kwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

Kuongeza matumizi ya simu janja ni moja ya chachu kwa Vodacom kufikia mafanikio ya azma yake ya kuifanya Tanzania kuwa ya kidijitali. Inalenga kutoa simujanja zenye ubora na kwa gharama nafuu.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Mauzo na Usambazaji wa Vodacom Tanzania, George Lugata alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa: "Tuna historia kubwa katika uendelezaji na uongezaji wa upatikanaji wa huduma za kiteknolojia kupitia simu. Tunaishi katika ulimwengu unaotaka kutuunganisha pamoja ambapo simu za kisasa sio anasa tena; bali ni hitaji muhimu la kiuchumi.

"Simujanja huwawezesha watu kuwasiliana, kujenga urafiki na pia kunufaika na fursa kadha wa kadha zinazotuzunguka kulinganisha na kipindi cha nyuma."

Lugata alisema wanaamini kuwa kila mtu anastahili kumiliki simujanja zenye ubora na ndio sababu kampuni hiyo inakuja na uvumbuzi mbalimbali ili kumwezesha kila mtanzania kumiliki simujanja.

Alisema kampuni itatoa zawadi kwa wateja watakaonunua simu hiyo, ikiwa ni pamoja na GB 96 kwa muda wa miezi 12 ili kufurahia huduma za kidijitali wanazozitoa.

Alisema kuwa Vodacom kwa kushirikiana na Infinix wataendesha kampeni 'Chemsha Bongo' kwa vyuo vinne vya elimu ya juu vilivyopo Dar es Salaam ambavyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Benno Malisa (wa tatu kushoto) akifungua pazia kuashiria uzinduzi wa tawi jipya la Benki ya NBC eneo la Mwanjelwa mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mjumbe wa Bodi ya NBC, Godfrey Malekano (wa tano kulia), Mkurugenzi Wateja Binafsi wa benki hiyo, Elibariki Masuke (wa tatu kulia), Mwenyekiti Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo, Dk. Kassim Hussein (kulia) na viongozi wengine waandamizi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yazindua tawi jipya jijini Mbeya

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imezindua tawi jipya eneo la Mwanjelwa mkoani Mbeya, uongozi wa serikali ukiwaita wafanyabiashara na wakazi wa mkoa huo kuchangamkia fursa za kiuwekezaji kiuchumi inazozitoa mkoani hapa.

Hafla ya uzinduzi wa tawi hilo uliofanyika mwishoni mwa wiki, iliongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya Mjini, Benno Malisa aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa, Juma Homera na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali, viongozi waandamizi wa benki hiyo na wafanyakazi, wawakilishi wa jumuiya ya wafanyabiashara na wananchi

Akizungumza kwa niaba ya Homera, Malisa alisema mitaji ya fedha ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya kiuchumi, hivyo kuwapo kwa NBC eneo hilo la Mwanjelwa kutakuwa na tija zaidi iwapo wakazi wataitumia vyema fursa hiyo.

"Ninajua fika kwamba kusogezwa karibu huduma za kifedha ikiwamo benki kama hivi ni jambo moja na kutumia ipasavyo kuwapo kwa huduma hizi ni jambo lingine.

"Ndiyo maana ninawaomba sana wananchi wa Mwanjelwa kutumia vyema fursa inayotolewa na Benki ya NBC kutunza akiba zenu na pia kukopa ili kuwekeza na kukuza biashara zenu," alisema.

Malisa alitoa rai kwa NBC kuendelea kubuni mipango mbalimbali ya utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutumia benki na kuongeza huduma zinazowagusa wananchi wenye hali ya kawaida kiuchumi ili wakuze uchumi binafsi na kupanua uchumi wa nchi.

"Ninafahamu Benki ya NBC mmekuwa mkibuni njia mbadala za kuwahudumia wateja kupitia njia mbalimbali ikiwamo kupitia mawakala na huduma kupitia simu, yaani NBC Kiganjani, NBC Shambani na nyingine nyingi.

"Ninawapongeza sana. Hata hivyo, ninaomba sana endeleeni kuwaelimisha wateja wenu namna ya kutumia fursa za kibenki na kujikomboa kiuchumi.

"Mkoa wa Mbeya kwa sasa unakua kwa kasi sana na wakazi wanaongezeka kila siku huku shughuli za kiuchumi pia zikiongezeka. Ongezeko hili la watu na ukuaji wa kiuchumi unahitaji kwenda sambamba na huduma mbalimbali ikiwamo hii ya kifedha. Tunawashukuru sana na NBC kwa kuliona hili na kutusogezea huduma za kifedha Mwanjelwa," alipongeza.

Akizungumza niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Mkurugenzi Wateja Binafsi wa benki hiyo, Elibariki Masuke alisema benki hiyo ambayo inamilikiwa na serikali kwa asilimia 30 inaendelea kuunga mkono dhamira ya serikali ya kuwawezesha wajasiriamali na wakulima na wazalishaji wengine katika sekta za uchumi kwa kutoa mitaji ya kifedha na mikopo nafuu.

"Jitihada hizi tunazitekeleza kwa urahisi zaidi kutokana wingi wa matawi yetu katika mikoa mbalimbali nchini. Tawi hili jipya la Mwanjelwa tunalolifungua leo linafanya benki sasa kuwa na jumla ya matawi mawili hapa Mbeya na hivyo na kufanya jumla ya matawi yetu kufika 52 kote nchini.

"Kupitia matawi haya tumekuwa tukihudumia makundi yote ya jamii ikiwamo taasisi za serikali, watumishi wa serikali, wakulima, wafanyabiashara, wanafunzi sambamba na kukusanya maduhuli ya serikali kupitia Mfumo wa Ukusanyaji wa Fedha za Umma (GePG) na kodi kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato (TRA)," alisema.

# SIMBA YAANIKA WACHEZAJI ITAKAOWASAJILI MSIMU UJAO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema kwa sasa imeamua kusaka wachezaji bora zaidi ili kuungana na waliopo kwa ajili ya kuwatoa hapo walipo na kuwapeleka hatua nyingine kubwa zaidi.

**Imeweka wazi kuwa tayari imeshaanza mchakato wa kufanya usajili wa wachezaji bora na wenye uwezo zaidi barani Afrika ambao wanawazidi hawa waliopo, baada ya misimu mitano ya kuishia hatua ya robo fainali, huku ikishindwa kuvuka hatua hiyo mara tatu Ligi ya Mabingwa Afrika na mara moja Kombe la Shirikisho barani Afrika.**

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kwa sasa wanasaka wachezaji watakaoweza kuwasaidia kuvuka kwenye hatua ya robo fainali na hata kutwaa ubingwa wa Afrika ili waje kuungana na hawa waliopo ambao ni wanarobo fainali.

Amekiri kuwa kwa kiasi kikubwa usajili wa msimu huu haukuwaridhisha viongozi wa klabu hiyo, hivyo kwa sasa wamejifunga vibwebwe kuhakikisha kiu ya wanachama na mashabiki wa Simba inaisha.

"Usajili mkubwa ambao tumeufanya msimu huu asilimia kubwa haujaenda vile ambavyo Simba tulihitaji na ndiyo maana tumeishia pale pale kwenye robo fainali. Kwa hiyo viongozi wetu walemeliona hilo na wao wanaumizwa na mgando huu tulionao na sasa wanapambana kuona kwamba tunatafuta wachezaji waliokuwa bora zaidi waweze kutupeleka katika hatua ambayo Wanasimba tunaihitaji.

"Tutafanya kila linalowezekana ili kutoka hapa tunapoishia kwa miaka mitano sasa. Tunafanya usajili uliokuwa bora, tutatafuta wachezaji watakaoweza kutusaidia kutoka hapa kwenda kwenye hatua inayofuata, wachezaji tuliokuwa nao hivi sasa pasi na shaka yoyote wanaweza kutufikisha robo fainali, hata Ligi ya Mabingwa ikianza hii leo,

"Tuna uwezo wa kucheza robo fainali, sasa nini kinatakiwa? Ni kusajili na kupata nyota wengine wapya wenye viwango bora na vya juu, kuja kuungana na hawa wanarobo fainali kuja kutupeleka nusu fainali na hata fainali," alisema Ahmed.

Alisema kwenye dirisha hili la usajili walifanya usajili wakiamini utakwenda kuwasaidia, lakini kwa bahati mbaya usajili siku zote ni kamari.

"Viongozi wetu waleliona na kulijua hilo na kwenye dirisha hili la usajili ndicho tunachoenda kufanya. Msimu huu tulifanya usajili tukiamini ya kwamba utakuja kutusaidia kutupeleka huko ambako tulikuwa tunakusudia, lakini nyote mnafahamu usajili ni kamari, unaweza kutoa mtu kwao ni mzuri tu na uwezo mkubwa, lakini akija hapa mambo yanamkataa," alisema Ahmed.

Mwaka 2019 Simba ilitolewa kwenye hatua kama hiyo Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ikifungwa ugenini mabao 4-1, baada ya suluhu ya nyumbani na 2021, ilichapwa mabao 4-0 dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, licha ya ushindi wa mabao 3-0 nyumbani haikutosha kuwapeleka nusu fainali na msimu huu imetolewa na Mabingwa Watetezi, Wydad Athletic Club ya Casablbca nchini Morocco kwa mikwaju ya penalti 4-3 baada ya kila timu kushinda bao 1-0 nyumbani.

Mwaka jana, Simba pia iliishia robo fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika ilipotolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3 na Orlando Pirates ya Afrika Kusini, baada ya kila kitu kushinda bao 1-0 nyumbani.

## TFF yashtukia upangaji matokeo Championship

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limesema linafuatilia kwa ukaribu suala la tuhuma za rushwa kwenye mechi ya Ligi ya Championship kati ya Fountain Gate FC na Kitayosce, iliyochezwa Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa CCM Gairo, Morogoro na timu hizo kutoka suluhu.

Taarifa iliyotolewa na TFF kupitia kwa Afisa Habari na Mawasiliano wake, Cliford Ndimbo, imeeleza kuwa Sekretarieti ya TFF itafanya uchunguzi wa tukio hilo hadi dakika za mwisho na itachukua hatua kwa mujibu wa taratibu za mpira wa miguu.

Ni mechi ambayo imeendelea kuiweka Kitayosce yenye maskani yake mkoani Tabora, kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 54, ikipigana vikumbo na Pamba ya Mwanza iliyopo nyuma yao na alama zake 53.

Ligi hiyo iliendelea tena juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba wakati wenyeji Copco ilipoichapa Green Warriors mabao 2-1.

Ni matokeo ambayo yanaifanya Copco kufikisha pointi 23 ikiwa kwenye nafasi ya 11, huku Green Warriors ikiwa nafasi ya 13 na pointi zake 23 pia, lakini timu hizo zimeachana kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

TFF ilitangaza kuwa itakuwa makini kwenye mechi za mwisho ambazo kuna timu zinazowania kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara, huku JKT Tanzania ikiwa tayari imepanda, na zingine zikicheza kuepuka kushuka daraja.

**TUPO TAYARI...**



Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira (kulia), akiwa na msaidizi wake, Ouanane Sellami, tayari kwa safari ya kuelekea Lindi kuiongoza timu yao kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Namungo FC, itakayopigwa kesho katika Uwanja wa Majaliwa. **MPIGAPICHA WETU**

## Mfaume ulingoni na bondia Msauzi

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Mfaume Mfaume 'Mapafu ya Mbwa', anatarajia kupanda ulingoni dhidi ya Nkululeko Mhlongo raia wa Afrika Kusini katika pambano linalotarajiwa kupigwa Juni 30, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Mfaume anarejea ulingoni katika pambano hilo lililopewa jina la "Hata usipo lala patakucha", ikiwa imepita miezi sita tangu alipozichapa Desemba mwaka jana katika pambano lililovunjika dhidi ya Idd Pialali kwa madai ya kupigana vichwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Kampuni ya Paf Promotion Entertainment Company Ltd, Fadhili Maogola, alisema bondia huyo atarejea ulingoni kwenye pambano walilomuandalia dhidi ya Nkululeko kutoka Afrika Kusini likiambatana na mapambano mengine ya utangulizi.

Alisema wameanza kazi ambayo waliahidi kwa muda mrefu wa kuanda pambano kali la kimataifa kati ya Mfaume na bondia huyo kutoka Afrika Kusini.

"Tumeanza maandalizi na tayari bondia ameshaingia kambini kufanya maandalizi pamoja na mabondia wengine ambao watacheza mapambano ya utangulizi, lakini kwa upande wetu tunaendelea na maandalizi pamoja na kutafuta wadhamini bado milango ya kudhamini ipo wazi, tunawakaribisha kwa wingi kwa sababu hii kwetu ni mara ya kwanza kufanya tukio la aina hii," alisema Maogola.

## Kundembwa yatupwa nje FA Cup Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kundemba FC imetolewa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, baada ya kukubali kipigo cha mabao 4-3 dhidi ya majirani zao, Mwembeladu FC, katika mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-bora uliopigwa juzi.

Kundemba FC inakuwa timu ya kwanza ya Ligi Kuu Zanzibar kuotolewa katika hatua hiyo na kushindwa kutinga robo fainali.

Akizungimza na gazeti hilo Kocha Mkuu wa Kundemba FC, Ali Vua Shein, alisema mechi ilikuwa ngumu na amekiri kuzidiwa katika dakika za mwisho za mchezo.

Alisema tangu hapo awali alijua mchezo huo walitakiwa wacheze kwa tahadhari kubwa, lakini ilionekana wapinzani wao waliwasoma mbinu zao mapema.

"Lengo katika michuano hii ya FA ni kutinga fainali, lakini haikuwa bahati kwetu tumetolewa mapema, hivyo kilichabaki ni kuhakikisha nguvu zetu tunazipeleka katika michezo ya Ligi Kuu iliyobaki ili tuweze kufanya vizuri," alisema.

## ZISIKUPITE

### HAALAND MKATABA MPYA

KLABU ya Manchester City inajiandaa kufanya mazungumzo na mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland, mwenye umri wa miaka 22, kuhusu mkataba mpya. ***(Football Insider)***

### ZAHA ANAHUSUDIWA

MSHAMBULIAJI wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha anahusudiwa na Klabu za Arsenal, Juventus, Chelsea na Barcelona huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, akitarajiwa kuondoka Selhurst Park mwishoni mwa msimu mkataba wake unapomalizika. ***(Telegraph)***

### MOUNT KUBAKI CHELSEA

KLABU ya Chelsea ina imani kuwa kiungo wake wa kati wa England, Mason Mount, mwenye umri wa miaka 24, atazikataa Bayern Munich na Liverpool na kusaini mkataba mpya ili kusalia katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

### KUPELEKWA SOKONI

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Dusan Vlahovic, mwenye umri wa miaka 23, anataka kuuzwa kwenda Arsenal au Bayern Munich huku muda wa Mserbia huyo katika klabu hiyo ya Italia ukionekana umefikia mwisho ***(Tutto Mercato Web)***

### EVANS AFUATILIWA EPL

CHELSEA ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinazomfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa kati wa Stevenage, Makise Evans mwenye umri wa miaka 16. ***(Sun)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inafikiria kumnunua mshambuliaji wa AS Roma mwenye umri wa miaka 29 kutoka Argentina Paulo Dybala. ***(Calcio Mercato)***

### HAKIMI AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili beki wa pembeni wa Paris St-Germain, Achraf Hakimi, 24. ***(Football Insider)***

### MCBURNIE KUONGEZEWA

SHEFFIELD United iko tayari kumuongezea mkataba mshambuliaji wa Scotland, Oli McBurnie, mwenye umri wa miaka 26, baada ya kufanikiwa kupanda daraja kucheza Ligi Kuu England msimu ujao. ***(Sun)***

### MANE ATAJWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea inahusishwa na mshambuliaji wa Bayern Munich na Senegal, Sadio Mane, mwenye umri wa miaka 31, ambaye alijiunga na timu hiyo ya Ujerumani akitokea Liverpool msimu uliopita wa majira ya joto. ***(Football London)***

### TELLES AWINDWA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia, Al Nassr inamfuatilia beki wa kushoto wa Brazil, Alex Telles, mwenye umri wa miaka 30, ambaye yuko kwa mkopo Sevilla akitokea Manchester United na huenda akaungana tena na mchezaji mwenzake wa zamani wa 'Mashetani Wekundu', Cristiano Ronaldo. ***(AS)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG: BRUNO NDIYE NAHODHA BORA ZAIDI

**MANCHESTER,** England

**Anaipa timu nguvu nyingi zaidi ya ujanja wake, lakini pia dhamira yake, mapenzi yake na...**

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amesema kiwango alichoonesha, Bruno Fernandes, kwenye mechi ya ushindi dhidi ya Aston Villa kimeonesha jinsi gani mjadala wa hivi karibuni kuhusu unahodha wake ulivyokuwa "wa kichaa".

**'Mashetani Wekundu' walijiimarisha katika nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumapili, wakati bao la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, katika kipindi cha kwanza lilitosha kuwapatia ushindi wa 1-0 pale Old Trafford.**

Ilikuwa ni moja ya kiwango bora na chakuvutia cha Fernandes, ambaye kwa namna fulani alipona kutokana na kuendeleza malalamiko ya kifundo cha mguu alichoumia katika nusu fainali ya Kombe la FA Jumapili iliyopita dhidi ya Brighton.

Ten Hag alimwagia sifa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno baada ya sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tottenham, akimwita "msukumo" na mfano ambao wachezaji wenzake wanapaswa kufuata.

Kocha huyo wa United alitoa sifa zile zile Jumapili na akataja jinsi mazungumzo ya kuchekesha kuhusu kufaa kwake unahodha yalivyokuwa kutokana na kipigo cha mabao 7-0 kutoka kwa Liverpool.

Alipoulizwa kuhusu uthabiti wa Fernandes kucheza baada ya wiki moja ya kugongwa kwa kifundo cha mguu, Ten Hag alisema:

"Yeye ni mgumu sana. Wiki chache zilizopita kulikuwa na maswali kuhusu unahodha wake. Ni kichaa kwa sababu yeye ni kiongozi mkubwa na wa mfano.

"Anaipa timu nguvu nyingi zaidi ya ujanja wake. "Lakini pia dhamira yake, mapenzi yake na uimara wake, kwa hiyo nadhani sisi kama timu tuna furaha sana.

"Tunahitaji wachezaji kama hao ikiwa unataka kushinda michezo, ikiwa unataka kushinda mataji."

Ten Hag aliongeza: "Ni furaha kufanya kazi na wachezaji kama Fernandes, ambaye alikuwa nahodha tena huku Harry Maguire akiwa benchi na kuwapa United ushindi ambao unawaweka katika nafasi nzuri ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Lazima tuendelee kutoka mchezo hadi mchezo, lakini nadhani hii ni wiki nzuri kwetu," alisema Mholanzi huyo.

"Unapokuwa kwenye nusu fainali katika mchezo mgumu dhidi ya mpinzani mzuri (Brighton) kama tulivyoona katikati ya wiki, tulicheza mchezo mzuri sana na kufika fainali.

"Kisha Tottenham, katika kipindi cha kwanza tulicheza vizuri sana na leo (juzi) tulicheza mchezo wa kuvutia, sifa kubwa kwa timu."

United wanaelekea Brighton Alhamisi usiku wakitafuta kudumisha kasi, huku Villa wakiwa na nafasi ya kurejea kutoka kupoteza kwa mara ya kwanza ndani ya wiki 10 wakiwa Wolves Jumamosi.

Vijana wa Emery wanamaliza wikendi wakiwa nafasi ya saba kwenye msimamo na mshindi huyo mara nne wa Ligi ya Europa hajakata tamaa katika kufuzu kucheza michuano ya Ulaya.

"Ni ngumu zaidi unapojaribu kuwa katika 10 bora," bosi wa Villa alisema.

"Lakini ni ngumu sana unapotaka kuwa katika nafasi za Ulaya kwa sababu lazima ushinde na kushinda na kushinda.

"Tulikuwa tukifanya hivyo, lakini sasa tunapaswa kufanya hivyo tena. Hiyo ni hatua ngumu zaidi mbele ambayo tunayo, lakini tunastahili.

"Leo (juzi) dhidi ya Manchester United hatukucheza kwa ushindani kama tulivyofanya katika mechi zingine."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 567,
MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
CHELSEA
1 | 1.67
X | 3.67
2 | 4.57
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HAKIMI AMKERA KOCHA PSG

**PARIS,** Ufaransa

KADI nyekundu ya Achraf Hakimi wakati Paris Saint-Germain wakichezea kichapo kutoka kwa Lorient ilikuwa "ya kijinga sana", kwa mujibu wa kocha Christophe Galtier, ambaye anataka kikosi chake kiwe na malengo makubwa zaidi.

Mabingwa hao wa Ligue 1 waliteleza kwa kichapo cha mabao 3-1 baada ya kumpoteza Hakimi ndani ya dakika 20 za kwanza kwa kosa la pili la kadi ya njano.

Kupoteza huko kunaiacha PSG ikiwa bado inaongoza kwa alama tano kwenye msimamo wa ligi baada ya wapinzani wao Marseille kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Auxerre baadaye Jumapili.

Akitafakari nyekundu ya Hakimi, ambayo ilikuja baada ya kuwafanyia madhambi Romain Faivre na Darlin Yongwa, Galtier alikiri kukerwa kwake na mchezaji huyo na uchezaji wa timu yake.


"Hakukuwa na sababu kwa Achraf," alisema. "Kadi ya pili ni ya kijinga sana. Hakukuwa na dalili wiki hii kwamba atakuwa na wasiwasi.

"Inasikitisha sana, na inabidi tuchukue hatua haraka kwa sababu hatujui ni pointi ngapi tutakuwa nazo. Nusu yetu ya pili ya msimu imekuwa mbaya sana.

"Kuna haja ya kuwa na umoja lakini pia mwamko wa mtu binafsi. Wachezaji wengi sana wanaangalia ndani. Lazima tuangalie mbele.

"Mechi ya Troyes inakuja. Tumekuwa wa kwanza tangu kuanza kwa michuano, lakini tunapaswa kumaliza na ushindi. Tuna nia ya kufanya zaidi."




## Klopp alia na mwamuzi Tierney

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amembwatukia mwamuzi Paul Tierney baada ya kufanya msururu wa maamuzi tata katika ushindi wa Liverpool wa 4-3 dhidi ya Tottenham Hotspur, akisema: "Kwa kweli sijui mtu huyu ana nini dhidi yetu."

Wakiwa wametazamia kupata ushindi wa kawaida walipofunga mara tatu ndani ya dakika 15 za kwanza, Liverpool walipoteza uongozi wao kabla ya kupata ushindi wa dakika za lala salama.

Diogo Jota alitumia makosa ya Lucas Moura kupachika bao la ushindi, jambo lililomfanya Klopp afurahie mbele ya ofisa wa nne - kitendo ambacho kilimfanya bosi huyo wa 'Wekundu' hao kuumia mguu na kupewa kadi ya njano kutoka kwa Tierney.

Klopp alikasirishwa na uamuzi wa Tierney kutoa faulo dhidi ya Mohamed Salah katika maandalizi ya bao la kusawazisha la Tottenham, ingawa mchezaji wake mwingine Ryan Mason alihisi Jota angetolewa mapema kwa kumpiga Oliver Skipp kichwani.

Akikumbuka kushindw kwa Tierney kumtoa kw kadi nyekundu mshamb liaji wa Tottenham, Har Kane, walipokutana mw ka 2021 kati ya timu hiz Klopp alisema mwamu huyo ana "historia" na Li erpool.

"Ilikuwa hisia sana, bi shaka, hasa hali kabla bao lao la tatu," Klopp al iambia Sky Sports.

"Wanawezaje kumfan ia madhambi Salah mbel Mchezaji wa mstari yup moja kwa moja na anaw ka bendera yake chini.

,947,180

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/05/23 | 20:00 | Mjallby vs AIK Football | 2.77 | 2.93 | 2.45 |
| 02. 03/05/23 | 20:00 | Sparta Prague vs Slavia Prague | 2.31 | 3.22 | 2.80 |
| 03. 03/05/23 | 20:00 | Panathinaikos vs PAOK | 2.29 | 2.98 | 3.30 |
| 04. 03/05/23 | 20:30 | Valencia vs Villarreal | 2.90 | 3.30 | 2.26 |
| 05. 03/05/23 | 21:45 | Stuttgart vs Eintracht Frankfurt | 2.42 | 3.39 | 2.85 |
| 06. 03/05/23 | 21:45 | Burton vs Cambridge Utd | 2.97 | 3.22 | 2.31 |
| 07. 03/05/23 | 23:00 | Getafe vs Celta Vigo | 2.50 | 2.90 | 2.90 |
| 08. 04/05/23 | 01:00 | CD Palestino vs San Lorenzo | 2.90 | 3.01 | 2.36 |
| 09. 04/05/23 | 03:00 | Colo Colo vs Boca Juniors | 2.37 | 3.08 | 2.83 |
| 10. 04/05/23 | 03:00 | Club Guarani vs SC Emelec | 2.37 | 3.11 | 2.80 |
| 11. 04/05/23 | 20:00 | Norrkoping vs Hammarby | 2.52 | 3.33 | 2.42 |
| 12. 04/05/23 | 21:45 | Empoli vs Bologna | 2.95 | 3.10 | 2.33 |
| 13. 04/05/23 | 21:45 | Huddersfield vs Sheffield Utd | 2.45 | 3.20 | 2.70 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 02/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:30 | 2506 | Sunshine Coast Wanderers vs Redlands Utd | 2.28 | 3.53 | 2.65 |
| 13:00 | 2813 | Jeonnam Dragons vs Busan I Park | 2.39 | 3.08 | 2.72 |
| 13:00 | 2976 | Cheonan City FC vs Anyang | 4.21 | 3.69 | 1.66 |
| 13:00 | 5197 | Gangwon vs Cheongju FC | 1.53 | 3.95 | 5.20 |
| 13:30 | 1702 | Bucheon vs Chungnam Asan | 2.43 | 2.97 | 2.77 |
| 14:00 | 4806 | Barnsley U23 vs QPR U23 | 2.32 | 3.60 | 2.32 |
| 14:45 | 4761 | Anagennisi Karditsas vs Almopos Arideas | 1.62 | 3.21 | 5.79 |
| 14:45 | 4774 | Apollon 1926 vs PO Triglias | 4.24 | 2.95 | 1.90 |
| 15:00 | 2730 | Van Yerevan vs Urartu | 5.18 | 3.47 | 1.62 |
| 15:00 | 4122 | Bahir Dar Kenema FC vs Arba Minch Kenema | 1.66 | 3.42 | 4.87 |
| 16:00 | 2307 | Sheffield United U23 vs Colchester U21 | 1.32 | 4.70 | 5.80 |
| 16:00 | 4100 | Peterborough U21 vs Charlton U23 | 2.25 | 3.73 | 2.58 |
| 17:00 | 3103 | Lunca Teuz Cermei vs ACS Progresul Pecica | 2.51 | 3.37 | 2.47 |
| 17:00 | 3485 | Legia Warszawa vs Rakow Czestochowa | 2.97 | 3.18 | 2.23 |
| 17:00 | 5651 | Erzurum BB vs Sakaryaspor | 3.07 | 3.33 | 2.07 |
| 18:00 | 1683 | FC Politehnica Iasi vs FC Otelul Galati | 1.85 | 3.19 | 3.91 |
| 18:00 | 1776 | Javor Ivanjica vs FK Mladost Gat | 2.22 | 3.14 | 2.93 |
| 18:00 | 2000 | Ethiopia Bunna SC vs Adama City FC | 2.35 | 2.70 | 2.90 |
| 18:00 | 3986 | SK Super Nova vs FK Auda | 7.07 | 4.47 | 1.36 |
| 18:00 | 4036 | Rustaq Club vs Sur | 1.66 | 3.21 | 5.39 |
| 18:00 | 4371 | Pribram vs Slavia Prague B | 1.66 | 3.69 | 4.21 |
| 18:00 | 4555 | Dziugas vs FC Hegelmann Litauen Kaunas | 6.17 | 4.11 | 1.42 |
| 18:00 | 5378 | CS Blejoi vs FC Brasov | 1.75 | 3.58 | 3.99 |
| 19:00 | 1831 | Al Raed Club vs AL Baten | 1.58 | 4.16 | 5.12 |
| 19:00 | 2252 | Ghazl EL Mahallah vs Smouha Club | 3.71 | 2.86 | 2.15 |
| 19:00 | 2888 | Energie Cottbus vs Berliner Dynamo | 1.56 | 4.04 | 4.77 |
| 19:00 | 4060 | Shirak Gyumri vs Pyunik Yerevan | 8.20 | 4.40 | 1.26 |
| 19:00 | 5122 | Neftchi Baku vs Karabakh | 4.77 | 3.73 | 1.61 |
| 19:00 | 5345 | Abha vs AL Adalh | 2.07 | 3.46 | 3.36 |
| 19:30 | 3728 | FC Versailles 78 vs Red Star | 2.59 | 3.08 | 2.67 |
| 20:00 | 1678 | UTA Arad vs Hermanstadt | 2.07 | 3.08 | 3.55 |
| 20:00 | 3206 | Kristianstads FF vs IFK Trelleborg | 1.76 | 3.58 | 3.94 |
| 20:00 | 5066 | Helsingborg vs Gais | 2.93 | 3.36 | 2.32 |
| 20:30 | 2642 | Barcelona vs Osasuna | 1.22 | 5.35 | 11.59 |
| 20:30 | 3492 | Almeria vs Elche | 1.66 | 3.84 | 4.38 |
| 20:30 | 3796 | SuperSport Utd vs Stellenbosch | 1.98 | 3.14 | 3.77 |
| 20:30 | 4151 | FC Ashdod vs Maccabi Netanya | 2.48 | 3.15 | 2.64 |
| 21:15 | 3325 | Maribor vs NK Mura | 1.61 | 3.65 | 4.63 |
| 21:30 | 2672 | AL Tai vs AL Faiha | 2.07 | 3.52 | 3.31 |
| 21:30 | 2981 | Al Khaleej Club vs Al-Ettifaq | 2.77 | 3.25 | 2.49 |
| 21:30 | 3385 | Chelmsford vs St.Albans | 2.51 | 3.31 | 2.51 |
| 21:45 | 1505 | SC Freiburg vs RB Leipzig | 3.38 | 3.54 | 2.08 |
| 21:45 | 2478 | Shrewsbury vs Bristol Rovers | 2.26 | 3.32 | 2.97 |
| 21:45 | 5121 | Barnet vs Boreham Wood | 2.52 | 3.30 | 2.60 |
| 21:45 | 5727 | Alfreton vs Kidderminster | 2.54 | 3.21 | 2.54 |
| 22:00 | 2540 | Toulouse vs Lens | 4.09 | 3.75 | 1.73 |
| 22:00 | 2764 | Arsenal vs Chelsea | 1.66 | 3.67 | 4.68 |
| 22:00 | 5786 | Always Ready vs CD Real Tomayapo | 1.27 | 5.06 | 8.68 |
| 23:00 | 4964 | FC Aguablanca vs Universitario Popayan | 1.97 | 3.12 | 3.69 |
| 23:00 | 5523 | Real Sociedad vs Real Madrid | 2.41 | 3.29 | 2.69 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KUZIMIKA TAA YANGA, RIVERS UNITED KWAONDOA 7 KAZINI

**Na Adam Fungamwango**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, ameelekeza kusimamishwa kazi wafanyakazi saba wa Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam kutokana na jenereta la uwanjani hapo kushindwa kufanya kazi juzi wakati wa mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kati ya Yanga na Rivers United ya Nigeria.

**Waliosimamishwa kazi ni Salum Mtumbuka ambaye ni Kaimu Meneja wa uwanja, Manyori Juma Kapesa ambaye ni Mhandisi wa Umeme na Tuswege Nikupala ambaye ni Afisa Tawala wa uwanja huo.**

Taarifa iliyotolewa na Kitendo cha Mawasiliano Serikalini kwenye Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo chini ya Eleuteri Mangi, imesema Waziri Chana amemuelekeza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Said Yakubu, kuwasimisha kazi wahusika ili kupisha uchunguzi kwa wafanyakazi wanaohusika na uendeshaji mwanga.

Aidha, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, pia amewasimamisha kazi wafanyakazi wengine ambao wana majukumu ya uendeshaji kwenye uwanja huo ambao ni Gordon Mwangamilo, Gabriel Mwasele, Yanuari Imboru na Dk. Christina Luambano.

Kufuatia hatua zilizochukuliwa, Katibu Mkuu, Yakubu amemteua Milinde Mahona kuwa Kaimu Meneja wa Uwanja wa Benjamin Mkapa na uteuzi huo unaanza mara moja.

Aidha, maagizo mengine ni Katibu Mkuu kuwasiliana na wadau wote husika ili mechi zitakazochezwa kwenye uwanja huo sasa zichezwe majira ya alasiri au jioni badala ya usiku katika kipindi ambacho wizara inakamilisha taratibu za kupata mzabuni atakayefanya ukarabati mkubwa kwenye uwanja huo kabla ya kuanza kwa msimu ujao wa ligi na michuano ya kimataifa.

Waziri pia ameagiza mamlaka za nje ya wizara kufanya uchunguzi wa kukatika umeme kwenye uwanja huo na kuchukua hatua.

Wizara pia imeomba radhi mashabiki wa soka nchini, hususan wa timu ya Yanga kwa kadhia iliyojitokeza, na imeahidi Watanzania wote kwamba itaendelea kufanya ukarabati mdogo na mkubwa ili uwanja huo uendelee kutoa huduma na burudani kwa Watanzania wote pamoja na nchi jirani zinazotumia uwanja huo.

Kwenye mechi hiyo ambayo ilimalizika kwa suluhu na Yanga kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali, baadhi ya taa za uwanja huo zilizimika na zingine kutoa mwanga hafifu saa moja na dakika 27 kwa saa za Afrika Mashariki na Kati, ikiwa ni dakika ya 27 ya mchezo, kama ilivyotokea Machi 28, mwaka huu kwenye mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kati ya wenyeji Tanzania, Taifa Stars dhidi ya Uganda, The Cranes.

Mechi ya Taifa Stars na Uganda ilisimama katika dakika ya 37, na iliendelea tena baada ya mambo kukaa vema dakika 35 baadaye, lakini kwenye mechi ya juzi mwanga wa taa ulirejea tena na mechi ikaendelea saa 20:00 usiku, ikiwa ni baada ya dakika 33 kupita.




## Chama awatuliza mashabiki Simba

INATOKA UK. 24

Kikosi cha Simba kimeondoka jana mchana kuelekea Lindi tayari kwa mchezo huo, ambapo baadaye kitaunganisha kwenda Mtwara kwa ajili ya kuivaa Azam FC kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA itakayopigwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona Jumamosi.

## *Nabi aigeukia Marumo*

INATOKA UKURASA 24

na kwamba mikakati aliyoingia nayo katika robo fainali itakuwa tofauti na atakavyocheza nusu fainali.

Kocha Mkuu wa Rivers United, Stanley Azunda Eguma, alisema matokeo ya kutolewa katika mashindano hayo si mazuri kwao huku akiipongeza Yanga kwa kusonga mbele.

Alisema mechi walishapoteza wakiwa kwao Nigeria baada ya kuruhusu kufungwa mabao 2-0, licha ya juzi kucheza kwa nidhamu na kutengeneza nafasi lakini wakashindwa kuzitumia.

"Kupoteza mabao 2-0 Nigeria ndio ilikuwa shinda, leo wachezaji walipambana kufikia malengo, lakini ilishindikana, sasa tunachukuwa mapungufu yetu na muda mwingine tutafanya vizuri," alisema Eguma.

# Michezo

Jumanne Mei 2, 2023

Nipashe




'Bruno ni nahodha bora zaidi' UKURASA 21

HUNIWEZI...



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akikokota mpira dhidi ya beki wa Rivers United kwenye mechi ya mkondo wa pili ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa sare tasa. **MPIGAPICHA WETU**

# Nabi aigeukia Marumo, kuzima taa kwaondoa 7

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## ●●● Ni wakati mechi ya Yanga na Rivers ikipigwa kwa Mkapa, serikali yatoa tamko mechi sasa mchana huku...

BAADA ya kutinga nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema hesabu zake sasa ni namna ya kuhakikisha anatinga fainali dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini ambao wametinga hatua hiyo kwa kupata matokeo ya jumla ya mabao 2-1 dhidi ya Pyramids ya Misri.

**Marumo ililazimisha sare ugenini ya bao 1-1 dhidi ya Pyramids kabla ya juzi ikiwa nyumbani Afrika Kusini kuibuka na ushindi wa bao 1-0, wakati Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 ugenini nchini Nigeria dhidi ya Rivers United na kisha kutoka suluhu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.**

Akizungumza na Nipashe juzi baada ya dakika 90, Nabi alisema mechi yao ilikuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu alitambua wapinzani wao hao wangekuja kucheza kwa kushambulia zaidi, hivyo ikamlazimu kucheza mfumo wa kuzuia zaidi.

"Mechi ilikuwa ngumu tangu awali nilisema kuwa Rivers hawana cha kupoteza wangecheza mpira, ikatulazimu kucheza kwa kuzuia kwa sababu ningefunguka wangepata bao la kwanza na baadaye wangefunga la pili.

"Hatukucheza kwa kukaba pekee, pia niliweka washambuliaji [wawili] ili tukipata nafasi tuweze kufunga na tulitengeneza nafasi mbili hatukuweza kuzitumia.

"Mechi iliyopita tulitengeneza nafasi mbili ugenini na kufanikiwa kushinda, hii tulitengeneza nafasi tano, lakini hatukuzitumia, tungefunguka basi tungepoteza mchezo. Hizi mechi nimewahi kushuhudia kushinda ugenini na kufungwa nyumbani," alisema kocha huyo.

Nabi alimkingia kifua mshambuliaji chipukizi, Clement Mzize, na kudai kuwa kushindwa kutumia nafasi walizotengeneza inatokana ni sula la kimpira na si kucheza chini.

"Mzize ni kijana wa Kitanzania na tegemeo la baadaye, kwangu hakucheza vibaya kwa sababu alipata nafasi mbili na kutozitumia vizuri, lakini nafasi kama hizi zinamjenga na kujiamini, kuhusu mikakati yangu ya hatua ya nusu fainali inaendelea.

"Sijajua hadi sasa (juzi) nakutana na nani kati ya Marumo Gallants au Pyramids, itanilazimu kabla ya kuanza mipango ya mechi hiyo lazima niwafuatilie wapinzani wangu ubora na madhaifu yao," alisema Nabi.

Aliongeza kuwa hatoishia kuangalia hayo, bali pia mbinu za kiufundi wanavyocheza ugenini na nyumbani wanakuwaje ili kuanza rasmi mipango yao kuelekea mchezo huo wa nusu fainali

"Kazi nitaanza kuifanya baada ya mchezo huu na kuona wapinzani wetu hao na kuanza kuangalia jinsi gani ya kujipanga na kuingia kwa mfumo gani katika mchezo wetu huo tutakaoanzia nyumbani," alisema Nabi.

Alisisitizia kuwa kila mechi wanaingia na mipango yake

INAENDELEA UKURASA 23

# Chama awatuliza mashabiki Simba

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Simba, Clatous Chama, amewatuliza mashabiki wa timu hiyo baada ya kudai kuwa matokeo waliyoyapata wikiendi hii ya kutolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ni chachu kwao ya kuendelea kuimarika kwa kikosi chao.

Simba imetolewa kwenye michuano hiyo nchini Morocco na Wydad Casablanca kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya kumaliza dakika 180 kwa sare ya bao 1-1, 90 za kwanza Simba ikishinda 1-0 nyumbani na kisha kupoteza kwa kipigo kama hicho ugenini.

Akizungumza na Nipashe jana, Chama alisema mashindano hayo yalikuwa ni safari ndefu yenye mambo mengi ndani yake, hisia mchanganyiko kuanzia mwanzo hatua ya makundi hadi kutolewa kwenye hatua ya robo fainali.

Alisema Ijumaa walifanya kila kitu wanachokijua lakini mwisho wa siku ilibidi wakubaliane na ukweli ili kuweza kusonga mbele, na bahati haikuwa kwao na sasa wanarudi kujipanga upya kwa msimu ujao.

"Shukrani za dhati kwa wachezaji, benchi la ufundi, Rais wa Heshima Mohamed 'Mo' Dewji na mashabiki, maombi na upendo wenu ndio umetufikisha hapa leo. Tutachukulia matokeo haya kama chachu ya kuendelea kuimarika , asanteni kwa ushauri na kutia moyo," alisema Chama.

Kiungo huyo alisema wachezaji walipambana na kujitoa zaidi katika mechi hiyo, lakini wakatolewa kwa mikwaju ya penalti na kwamba anaimani haikuwa bahati kwao, hivyo matokeo hayo kwao imekuwa ni sehemu kubwa ya wao kujifunza.

Aliongeza baada ya kutolewa kwenye michuano hiyo, sasa akili na nguvu zao wanazielekeza katika michezo iliyosalia ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo kesho watashuka Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi kuivaa Namungo FC kabla ya Jumamosi kucheza nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >